# Nipashe

Alhamisi Juni 18, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580261

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

215779502




## Wanafunzi 73,000 kujiunga kidato cha tano mwaka huu

UKURASA 3

### BAA LA CORONA



Kumbuka kuwa uvaaji wa barakoa pekee hauzuii maambukizi ya virusi vya corona kutoka kwako kwenda kwa wengine, njia nzuri za kujilinda na kuwalinda wengine dhidi ya Covid-19 ni usafi wa mikono yako.

- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

# Mbio za urais mshikemshike

- JPM atangulia CCM, Zanzibar wafikia 5, yumo Hussein Mwinyi. 11 watia nia CHADEMA, CUF yaweka kiporo... *Endelea Uk. 2,4*



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi CCM, Rais John Magufuli, akikabidhiwa fomu ya kuomba ridhaa ya kuteuliwa kugombea urais kutoka kwa Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally katika Ofisi za Makao Makuu ya CCM jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**.



Peter Msigwa



Tundu Lissu



Freeman Mbowe

## KIBANO CHAJA FEDHA ZA NGO

UKURASA 8

## Ndalichako aingilia kati ulipaji ada shule

UK. 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


MICHEZO **AZAM YASAKA MRITHI WA NGOMA** UK.23

MAONI, KATUNI UK.6

# JPM achukua fomu urais CCM

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli jana alikuwa mwanachama wa kwanza wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuchukua fomu ya kugombea tena urais kwa muhula mwingine kupitia CCM, katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ikulu jijini Dodoma kupitia Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa, Rais Magufuli alikabidhiwa fomu hiyo na Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally.

Wengine walioshuhudia ni Naibu Katibu Mkuu wa CCM (Bara), Rodrick Mpogolo na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC), Uchumi na Fedha, Dk. Frank Haule.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa fomu hizo na kulipia ada ya Sh. milioni moja, Rais Magufuli alikishukuru chama hicho kwa kumpa fomu hizo.

"Ninawaomba wana CCM na Watanzania wote waniombee katika safari yangu ya kuomba ridhaa ya kupeperusha bendera ya CCM katika kinyang'anyiro cha kugombea kiti cha urais," alisema.

Pia, aliwaomba wana CCM wamdhamini na washiriki katika mchakato wa uchaguzi kwa amani, utulivu na mshikamano.

Baada ya kukabidhiwa fomu hizo, alianza safari ya kutafuta wadhamini ambapo alikwenda Ofisi ya CCM mkoani Dodoma na kumkabidhi Katibu wa Mkoa, Jamila Yusuph, fomu ya wadhamini 25.

Rais Magufuli alikutana na wanachama wachache wa CCM waliokuwa katika Ofisi ya Makao Makuu na Ofisi ya Mkoa na kuwatakia heri katika mchakato wa uchaguzi unaoendelea na kuwataka waendelee kukiimarisha chama.

Dirisha la uchukuaji fomu lilifunguliwa Jumatatu ya wiki hii na linatarajia kuendelea hadi Juni 30 sambamba na utafutaji wa wadhamini mikoani.

"Ndani ya siku 15 mgombea wa CCM atakuwa na kazi ya kuchukua fomu na kutafuta wadhamini mikoani na akamilishe kwa muda huo," alisema Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Humphrey Polepole.

Baada ya mchakato huo, kitakachofuata ni vikao vya uchujaji majina ya wagombea, vitakavyoanza Julai 6 hadi 7, mwaka huu.

Kikao cha Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya

CCM, kitaanza mchakato wa uchujaji wa majina ya wagombea na kuanza

Julai 8, kikao cha kamati ya usalama na maadili ya chama hicho. Julai 9, mwaka huu, kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, kitafanyika na kutoa mapendekezo ya majina matano ya walioomba kugombea nafasi hiyo kwa halmashauri kuu ya taifa ya CCM na Julai 10 halmashauri kuu ya taifa ya CCM, itapendekeza majina matatu ya wanachama walioomba kugombea nafasi hiyo kwa mkutano mkuu wa CCM.



Katibu wa Oganaizesheni ya CCM Zanzibar, Garlo's Nyimbo, akimkabidhi nyaraka mbalimbali kada wa CCM ambaye ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi, alipokwenda kuchukua fomu ya kuomba ridhaa ya kuteuliwa na chama hicho kugombea urais wa Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mbio za kumrithi Shein zashika kasi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADA ya Jumatatu pazia la mbio za urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kufunguliwa na makada wawili kuchukua fomu, jana mbio hizo zilishika kasi, baada ya wanachama watatu kujitokeza.

Waliojitokeza jana kumrithi Rais anayemaliza muda wake, Dk. Ali Mohamed Shein, ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Dk. Hussein Mwinyi, Omar Sheha Mussa na Mbwana Yahya.

Dk. Mwinyi alijitokeza kimyakimya katika ofisi za CCM Kisiwandui na kuchukua fomu.

Mwinyi sasa anaungana na makada wengine wanne ambao hadi jana walikuwa wamechukua fomu za kuomba ridhaa ya chama chao kupeperusha bendera yake katika uchaguzi mkuu uwa Oktoba mwaka huu.

Mwinyi ambaye hakutaka kuzungumza na vyombo vya habari baada ya kuchukua fomu hizo jana saa 7:30 mchana, mbali tu ya kupigwa picha, ni miongoni mwa Wazanzibar ambao wamekuwa wakitajwa sana kwamba angejitokeza kuomba uteuzi wa CCM.

Dk. Mwinyi ambaye ni mtoto wa Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ali Hassan Mwinyi, aliingia rasmi katika siasa za ushindani mwaka 1995 alipogombea ubunge katika Jimbo la Mkuranga mkoani Pwani kisha kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Afya katika serikali iliyoundwa na Rais Benjamin Mkapa. Tangu wakati huo sura ya Hussein Mwinyi haijawahi kukosekana kwenye Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano.

Hussein Mwinyi amedumu katika serikali tatu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika serikali ya awamu ya tatu ya Rais Mkapa, serikali ya awamu ya nne ya Rais Jakaya Kikwete na sasa Serikali ya Rais John Magufuli. Kwa sasa ndiye waziri mwandamizi kuliko wengine wote katika Baraza la Mawaziri.

Mwaka 1995, Hussein Mwinyi alikuwa kwenye kundi la vijana waliobuliwa na Rais Mkapa kupewa nafasi za unaibu waziri pamoja na Rais Magufuli na Waziri wa sasa wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi.

Hussein Mwinyi amehudumu katika Wizara ya Afya, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) na sasa Wizara ya Ulinzi na JKT.

Wakati wa kuchukua fomu jana, Dk. Hussein Mwinyi hakufuatana na wapambe alipowasili katika ofisi za CCM Kisiwandui akiwa ndani ya gari namba za kiraia. T151ADFA Toyota Land Cruiser.

**AKATAA KUZUNGUMZA**

Baada ya kuchukua fomu, alisema haikuwa siku yake ya kuzungumza na waandishi wa habari kwa kuwa ndiyo kwanza amechukua fomu, na sharti kwanza akazisome na kujua zinahitaji nini cha kufanya, na kwamba baada ya hapo atapata wasaa wa kuzungumza nao.

Hata hivyo, alikishukuru chama chake kwa kuruhusu demokrasia katika mchakato wa kutafuta viongozi wake, na ndio maana ametumia fursa hiyo kujitosa ulingoni.

Utaratibu wake wa kuchukua fomu unafanana na alioutumia Rais Magufuli mwaka 2015, kwa kutotaka kuzungumza chochote na wanahabari.

Rais Magufuli baada ya kupewa fomu, aliwaomba radhi wanahabari kwamba hakufika katika ofisi za CCM makao makuu Dodoma kuzungumza nao bali kuchukua fomu.

Pia aliwaeleza kuwa, ndiyo kwanza alikuwa amepewa fomu na maelezo yake, hivyo alihitaji muda wa kusoma na kutekeleza yaliyopo kabla ya kusema lolote.

**OMAR SHEHA MUSSA**

Omar Sheha Mussa, ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Chumbuni, akizungumzia vipaumbele ambavyo atavitekeleza kama atateuliwa na kuchaguliwa kuwa rais, atahakikisha anainua uchumi wa Zanzibar kwa kiwango kikubwa.

Alisema njia ambazo atazitumia katika kukuza uchumi huo ni pamoja na kuongeza mapato yatokanayo na biashara ya utalii, kujenga miundombinu itakayowezesha mapato hayo na kukuaji wa rasilimali akitolea mfano Bandari mpya ya Mpiga Duri.

Aidha alisema mbali ya Bandari hiyo ya Unguja, pia Pemba nako atashughulikia, mambo mengine ikiwamo kufanya upanuzi wa viwanja vya ndege kuwa vya kibiashara na kuongeza ajira kwa vijana.

Alisema mambo mengine ni kujenga bandari ya mafuta safi na ghafi pamoja kujenga miundombinu ya kuwezesha biashara hiyo ya mafuta.

"Nitajenga bandari ya mafuta na gesi katika maeneo yaliokwishateuliwa na serikali, mfano Mangapwani, kujenga bohari ya matangi ya hifadhi ya mafuta katika eneo hilo kwa lengo la kuongeza mapato ya serikali yatakayokusanywa eneo hilo," alisema.

Mussa alisema mambo mengine ni kusimamia utawala bora serikalini na taasisi zake kwa kutovumilia uzembe, wizi, rushwa hasa katika kuangalia utekelezaji wa majukumu waliyokabidhiwa.

"Lengo langu ni kuhakikisha nidhamu ya kazi na mwishowe kuleta tija na ufanisi katika usimamizi na utendaji kazi serikalini," alisema.

Alisema suala la kuwatetea na kuwasimamia wanyonge nalo atalipa kiumbele zaidi kwa kuhakikisha kila mwananchi anapata haki yake ikiwamo ya umiliki wa ardhi kwa mujibu wa sheria za Zanzibar.

Alieleza kuwa kipaumbele kingine ni kuleta mabadiliko katika kuunda serikali yenye lengo jipya na kujenga uwezo utakaobadili mwendendo wa kusimamia na kuendesha Zanzibar kwa mtazamo wakisiasa kama ilani ya CCM itakavyoeleza.

**MBWANA YAHYA MWINYI**

Kwa upande wake, mgombea mwingine, Mbwana Yahya Mwinyi, alisema, alifikia uamuzi wa kuchukua fomu hiyo, baada ya kujiona kwa ana kila kigezo cha kuiongoza Zanzibar kupitia nafasi ya urais.

"Nilijipima vyema na nimejitathmini hadi kufikia uamuzi huu ya kugombea nafasi hii ambayo katika katiba ya CCM imetoa fursa kwa kila kada mwenye vigezo husika kuwania nafasi hiyo," alisema.

Mbwana alisema endapo CCM itampa ridhaa ya kupeperusha bendera ya CCM, ataulinda Muungano na kuutetea kwa nguvu zote na kwamba ataitumia ilani ya uchaguzi wa CCM.

Makada wawili waliojitokeza Jumatatu ni Balozi Ali Karume na Mbwana Juma Bakari, ambao nao walieleza vipaumbele vyao kama watateuliwa na kuchaguliwa kuiongoza Zanzibar.

# 73,101 kujiunga kidato cha 5

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ametangaza kuchaguliwa kwa wanafunzi 73,101 kujiunga na kidato cha tano mwaka 2020.

Jafo amesema idadi hiyo ni kati ya wanafunzi 121,251, wengine wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya ualimu na vyuo vya ufundi vinavyosimamiwa na Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE).

Hata hivyo, amewataka wanafunzi wote wa bweni kuripoti shuleni Julai 18, mwaka huu na masomo yataanza rasmi Julai 20, mwaka huu huku akiwatahadharisha watakaoshindwa kuripoti ndani ya wiki mbili tangu shule kufunguliwa nafasi zao zitachukuliwa na wengine.

Alitangaza hatua hiyo jana, na kueleza kuwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano ni kutoka shule za serikali, zisizo za serikali, waliosoma nje ya mfumo rasmi na waliosoma nje ya nchi baada ya matokeo yao kupata ulinganifu wa Baraza la Mitihani Tanzania.

Alisema shule 434 zikiwamo shule 32 mpya za kidato cha tano zilizoanza mwaka huu zimepangiwa wanafunzi.

Alisema kati ya wanafunzi hao wa kidato cha tano waliochaguliwa wasichana ni 35,005 na wavulana 38,096.

Kati yao wanafunzi 1,572 wamechaguliwa kujiunga na shule za wanafunzi wenye ufaulu mzuri zaidi (vipaji maalum) ikiwamo wanafunzi 4 wavulana wenye mahitaji maalum.

"Pia katika uchaguzi huu wanafunzi 183 wa mahitaji maalumu, ambapo wasichana wakiwa ni 82 na wavulana ni 101," alisema. Kuhusu vyuo, Jafo alisema jumla ya wanafunzi 9,264 wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya elimu ya ufundi, vyuo vya afya na vyuo vya ualimu katika ngazi ya stashahada.

Wanafunzi 38,886 wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya elimu ya ufundi vinavyosimamia na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na wamepangwa katika vyuo na taasisi mbalimbali kama vile ardhi, biashara, maendeleo ya jamii, uvuvi, mifugo, kilimo, mazingira, mipango ya maendeleo vijijini. Alisema wanafunzi ambao hawataripoti wiki mbili tangu tarehe ya kufungua shule nafasi zao zitachukuliwa na wanafunzi wengine ambao hawakupangiwa shule katika awamu hii.

"Uhamisho wa shule hautaruhusiwa baada ya kukamilika kwa muhula wa kwanza wa masomo, na zoezi hilo litafanyika kwa kuzingatia uwepo wa nafasi kwenye shule kwa idhini ya maofisa elimu wa mkoa husika," alisema.

Aidha, alisema hakutakuwa na fursa ya kufanya mabadiliko yoyote ya shule kwa sasa ngazi ya mikoa halmashauri na shule.

Kadhalika, alisema wanafunzi waliopangwa kwenye vyuo vya elimu ya ufundi wanatakiwa kuthibitisha kukubali kujiunga na kozi zinazosimamiwa na NACTE baada ya siku saba kuanzia siku ya kutangaza kwa matokeo ya uchaguzi hadi Agosti 15 mwaka huu.

Alibainisha wanafunzi wanaotaka kufanya mabadiliko ya kozi au chuo walichochaguliwa wanaruhusiwa kufanya hivyo kuanzia Agosti 1 hadi 30 mwaka huu kupitia mtandao wa NACTE.

"Wanafunzi waliopangwa katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya hawatahusika na utaratibu wa kubadilisha wa NACTE, hivyo wanapaswa kuwasiliana na vyuo husika," alisema.



Wathamini wa Wizara ya Ardhi, Peter Mrema (kulia), na Adam Yusuph, wakisindikizwa kuingia Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, jana, kwa tuhuma za matumizi mabaya ya ofisi. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Ndalichako aingilia kati ulipaji ada shule

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ametaka busara kati ya wazazi na shule itumike katika ulipaji ada shule zitakapofunguliwa Juni 29, mwaka huu.

Pia, ametangaza mihula mipya ya masomo na ratiba ya mitihani kwa madarasa yenye mtihani huku akitaka shule kuongeza saa mbili za masomo kwa siku ili kufidia muda uliopotea.

Alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mihula hiyo na ratiba ya mitihani ya taifa kwa wanafunzi wa darasa la saba, nne, kidato cha nne na cha pili, jijini hapa.

Alisema ni vyema bodi za shule zikaweka utaratibu mzuri wa ulipaji ada kwa kuwa wakati janga la corona linatokea hakuna mtu aliyekuwa amejiandaa kukumbana nalo.

"Mi niseme ni vyema Watanzania tukapendana, hili ni janga hakuna mtu aliyekuwa anapenda litokee, na limeleta athari mbalimbali kuna wazazi wamepoteza kazi wenye watoto wanaosoma, shule nazo zilikuwa hazina wanafunzi zilifungwa kwa miezi mitatu, hili suala linahitaji busara itumike kuwapo na maridhiano kati ya mzazi na wamiliki wa shule," alisema.

Alitoa wito kwa wazazi ambao hawajakamilisha ada ya muhula wa kwanza wakamilishe, huku akikemea tabia ya shule kukataa kumpokea mtoto kwasababu ya kukosa ada.

"Tuweke ubinadamu tufikirie, sasa ulikuwa hujakamilisha ada ya muhula wa kwanza, shule zilisimama kwa miezi mitatu, huyo mwenye shule atajiendeshaje," alisema.

"Si vizuri shule kukataa kumpokea mtoto wa kitanzania kwasababu ya ada, ndio maana nasema ni vizuri kuwapo na maridhiano kwa pande zote wanaweza kuwekeana mkataba wa ulipaji."

Alisema muhula wa kwanza na wa pili umeunganishwa na kusisitiza kuwa suala la utaratibu wa ulipaji ada ni la bodi za shule huku akizitaka kuweka mfumo mzuri wa malipo ili ufanyike uamuzi wa kukubaliana.

"Tusianze kugawanyika kwasababu ya ada, na kusiwe na migogoro kwa sababu ya corona, busara itumike nisingependa kuwekwa utaratibu wa kila shule kulipa ada wakati tumekasimisha mamlaka kwa bodi za shule ambazo zipo kwa mujibu wa sheria," alisema.

**RATIBA YA MIHULA**

Kuhusu ratiba na mihula, Waziri Ndalichako alisema kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari watarejea Juni 29, mwaka huu kama ilivyotangazwa na Rais John Magufuli na kumaliza muhula wa kwanza wa masomo Agosti 28, mwaka huu.

"Muhula wa pili utaishia Desemba 18, mwaka 2020, ili kukamilisha muhtasari wa masomo shule zitalazimika kuongeza saa mbili za masomo kwa siku ili kufidia muda uliopotea," alisema.

Hata hivyo, alisema maelekezo hayo hayatahusu madarasa ya awali, darasa la kwanza na la pili.

Kuhusu wanafunzi wa kidato cha tano, alisema watasoma na kukamilisha muhtasari wa kidato cha tano na mitihani ifikapo Julai 24, mwaka 2020.

"Wanafunzi wataanza rasmi masomo yao ya kidato cha sita Julai 27, mwaka 2020," alisema.

**RATIBA ZA MITIHANI**

Akizungumzia ratiba ya mitihani, Prof. Ndalichako alisema darasa la saba watafanya mitihani yao Oktoba 7-8, mwaka huu, kidato cha pili Novemba 9-20, mwaka huu.

Aidha, alisema kidato cha nne watafanya mitihani yao kuanzia Novemba 23 hadi Desemba 11, mwaka huu na darasa la nne watafanya Novemba 25 hadi 26 mwaka huu.

Kuhusu tahadhari ya ugonjwa wa Corona, Prof. Ndalichako alisisitiza uongozi wa shule kuzingatia maelekezo ya kujikinga kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa hivi karibuni na Waziri wa Afya zilipofunguliwa shule za kidato cha sita na vyuo.

"Shule zihakikishe zinanunua vifaa vya kutosha kwa ajili ya kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, tuzingatie ili nchi iendelee kuwa salama,"alisema.

Kadhalika, alisema tangu kufunguliwa kwa shule kidato cha sita, hadi Juni 16, mwaka huu, hakijapatikana kisa hata kimoja cha mwanafunzi aliyepata Corona.

"Niwatakie kila la heri wanafunzi wote watakaorejea shuleni, tutawafuatilia kwa karibu na kuhakikisha masomo yanakweda vizuri, walimu wafundishe bila kukosa vipindi vyote na shule zizingatie maelekezo ya kujikinga na virusi vya Corona," alisema.

Alizitaka shule za bweni, ziweke utaratibu wa wanafunzi kufika mapema kati ya Juni 26-28 ili wajiandae kimasomo na kuepuka msongamano kwenye mabasi.

Kuhusu uvaaji barakoa, Waziri Ndalichako alisema Mwongozo uliotolewa na Waziri Afya umebainisha nani anapaswa kuvaa barakoa huku akizitaka shule zilizoshona kwa bei kubwa kutowalazimisha wazazi kununua bali zitoe uhuru wa mzazi kuamua.

"Watoto chini ya miaka mitano hawatakiwi kuvaa barakoa, pia walimu na wanafunzi wenye magonjwa kama ya moyo, pumu, nimonia, na mengine yameanishwa kwenye mwongozo kuhusu matumizi ya barakoa,"alisema.

# Watiania 11 kuchuana urais CHADEMA

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimepokea majina 11 ya watiania wa nafasi ya urais kupitia chama hicho waliowasilisha barua kuanzia Juni 3 hadi 15, mwaka huu.

Majina ya watiania hao ni Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, Makamu Mwenyekiti, Tundu Lissu, Mwenyekiti Kanda ya Nyasa, Peter Msigwa na Mwenyekiti Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu.

Wengine ni aliyekuwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita, Dk. Mayrose Majinge, Leonard Manyama, Gasper Mwanalyela, Opiyo Nalo, Shanani Msafiri na Neo Simba.

Mkuu wa Idara ya Mawasiliano wa chama hicho, Tumaini Makene, alitaja majina ya watia nia hao wakati akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam.

Alisema baada ya mchakato wa kupokea majina kukamilika Jumatatu, hatua inayofuata ni mchujo ambao utafanywa na kikao cha Kamati Kuu.

"Baada ya mchakato huu, tutaanza kuendelea na hatua nyingine kwa kuzingatia katiba na kanuni mbalimbali na majina ya watia nia yatawasilishwa katika vikao vya kamati kuu ya chama kwa ajili ya mchujo," alisema Makene.

Alisema mbali na watia nia hao 11, mmoja hakuingizwa kwenye orodha kutokana na kushindwa kukidhi vigezo.

"Kikundi cha madereva wa bodaboda kimejikusanya na kumjazia fomu mwanachama waliyeamini anafaa kuwania nafasi hii, lakini fomu ile haikukidhi vigezo kulingana na kanuni za CHADEMA, hivyo tumepokea barua za wanachama 11," alisema Makene.

Alieleza kuwa kati ya wagombea hao kila mtiania alijitokeza kwa wakati wake ndani ya muda uliopangwa kwa mujibu wa kifungu cha kwanza cha mwongozo cha kuwania nafasi ya uongozi serikalini.

Kuhusu mchakato baada ya kuanza kuchuja majina Makene alisema wakati wowote kuanzia sasa wataeleza hatua nyingine zitakazoendelea kufuata.

Kadhalika, Makene alipoulizwa utaratibu wa chama kwa hatua zinazofuata kumhusu mtiania Lissu aliyepo nje ya nchi, alisema chama kitatoa maelekezo isipokuwa kwa hatua za awali hazikumzuia kuwasilisha nia yake.



Ofisa Msimamizi wa Kodi wa TRA, Chama Siriwa, akitoa elimu ya kodi kwa mfanyabiashara wa eneo la Mji mdogo wa Mbalizi wakati wa kampeni kabambe ya uhamasishaji ulipaji kodi kabla ya tarehe 30 Juni, mwaka huu inayoendelea mkoani Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Mahakama yatoa siku 7 kesi ya Lissu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imetoa siku saba kwa upande wa Jamhuri kuwasilisha majibu ya kiapo kinzani na maombi ya wadhamini Ibrahim Ahmed na Robart Katula wa mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, Julai 14, mwaka huu.

Wadhamini hao amefungua maombi wakiiomba itoe hati ya kumkamata kwa kuwa wameshindwa kumpata na kumfikisha mahakamani hapo.

Maombi hayo yalipangwa kusikilizwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, lakini upande wa Jamhuri haujawasilisha majibu ya kiapo kinzani.

Hakimu Simba alisema mahakama yake itasikiliza maombi hayo Julai 14, mwaka huu na kesi ya msingi itatajwa siku hiyo.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba amri za awali kuhusu mshtakiwa Lissu zinaendelea.

Mbali na Lissu washtakiwa wengine ni Wahariri Simon Mkina, Jabir Idrisa na Mchapishaji wa Kampuni ya Jamana, Ismail Mehbooh.

Katika kesi ya msingi kwa pamoja washtakiwa hao, wanakabiliwa na mashtaka matano ikiwamo kuandika habari za uchochezi kinyume na Sheria ya Magazeti ya Mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari 12 hadi 14, 2016, jijini Dar es Salaam, washtakiwa Jabir, Mkina na Lissu, waliandika na kuchapisha taarifa za uchochezi zenye kichwa cha habari kisemacho, 'Machafuko yaja Zanzibar.'

Katika shtaka la pili wanadaiwa kuwa Januari 14, 2016 walichapisha habari hizo ili kuleta chuki kwa wananchi wa Zanzibar.

Mshtakiwa Mehbooh anadaiwa kuwa Januari 13, 2016 katika jengo la Jamana lililopo Manispaa ya Ilala, alichapisha gazeti la Mawio lililokuwa na taarifa za uchochezi.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo pia alichapisha gazeti hilo bila ya kuwasilisha hati ya sheria ya kiapo kwa Msajili wa Magazeti.

# CUF yaongeza muda watiania urais

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimesogeza muda wa watiania kwa nafasi ya urais hadi Juni 30, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi wa CUF Taifa, Juma Kilaghai, alisema wameamua kuongeza muda ili kutoa nafasi kwa watu wengi zaidi ambao walikuwa na nia ya kuwania kujipanga.

"Tumeona tusogeze mbele kwa sababu hapa katikati kulikuwa na mambo mengi na watu walikuwa na shughuli nyingi, kwa hiyo tunaamini mpaka Juni 30, watu watakuwa wametulia na kujitafakari zaidi na kufanya uamuzi uliyo sahihi,"alisema Kilaghai.

"Lakini pia hatuoni sababu ya kufunga haraka mchakato wa ndani wa chama, wakati hata Tume za Uchaguzi (NEC) na (ZEC) hazijafunga ratiba zake."

Awali, chama hicho kilitangaza kuwa mwisho wa uchukuaji na urejeshaji fomu kwa watia nia nafasi ya urais ni Juni 16.

Kilaghai alisema mpaka juzi waliokuwa wamejitokeza kutia nia katika nafasi hiyo ni wawili pekee, mmoja Tanzania Bara na mwingine Zanzibar.

**VYAMA KUUNGANA**

Akizungumzia ombi lao kwa vyama vyenye nia ya kuungana nao katika uchaguzi huo, Kilaghai alisema tayari kuna vyama vimejitokeza na wanafanya mazungumzo.

"Suala la vyama kuungana ni mchakato, siwezi kukuambia ni vyama gani ambavyo vimejitokeza mpaka sasa, lakini vipo na tunaendelea na mazungumzo,"alibainisha Kilaghai.

# TASAF kufanya uhakiki kaya maskini

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), unatarajia kuanza uhakiki wa kaya maskini kabla ya kuanza malipo ya awamu ya tatu kipindi cha pili katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

Taarifa hiyo ilitolewa jana mjini Mkuranga baada ya kufanyika kwa mafunzo kwa wawezeshaji watakaofanya kazi hiyo ngazi ya vijijini.

Uhakiki huo unatarajiwa kuanza hivi karibuni na utaondoa uwapo wa kaya ambazo hazijakidhi vigezo vya kuwa walengwa katika mpango huo.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa TASAF, Mery Mtambalike, alisema, katika kipindi cha pili cha awamu ya tatu kaya 1450,000 zenye watu zaidi ya milion saba kwa nchini zitanufaika.

Mtambalike alisema, mkazo mkubwa kwenye kipindi cha pili utalenga kuziwezesha kaya zitakazoandikishwa kwenye mpango kufanya kazi kuongeza kipato.

"Kipindi cha pili pia kitahakikisha huduma za jamii zinaongozwa na kuboreshwa ili kuendeleza rasilimali watoto hususani katika upatikanaji wa elimu na afya," alisema.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wazazi, walezi wanaweza kuepusha mimba za utotoni

**JANA** Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimetoa taarifa kwenye vyombo vya habari katika Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, kikieleza kuwa wanafunzi 100 wamepata mimba katika kipindi cha miezi mitatu ambacho walikuwa nyumbani kwa ajili ya janga la corona.

Aidha, kilieleza kuwa katika kipindi hicho zimeripotiwa ndoa nyingi za utotoni, jambo ambalo limechangia watoto wa kike kuendelea kurudishwa nyuma kielimu.

Kwamba kwa mwaka 2018/19 walipokea taarifa za kesi zaidi ya 2,540 za mimba za utotoni, na kwamba hali imekuwa mbaya zaidi kwa kipindi cha corona.

Pia, kilieleza kuendelea kuwapo kwa matukio ya walimu kujihusisha na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi wao, na katika kipindi hicho kilipokea kesi 24.

Matokeo ya utafiti wa LHRC yanatoa uhalisia wa wapi wazazi na walezi wamelega katika malezi ya watoto, kiasi cha kuonyesha kuwa inapotokea dharura ya watoto kulazimika kuwapo nyumba basi matukio ya ukatili dhidi yao unaongezeka.

Wanafunzi 100 kupata mimba kwa muda mfupi hivyo ni ishara mbaya kwa mustakabali na ustawi wa kitaaluma na maisha yao kwa ujumla, kwa kuwa ni rasmi kuwa ndoto za wasichana hao zimezikwa.

Sasa wanakwenda kuanza majukumu mapya ya kulea familia, kuwa mke wa fulani katika umri ambao walipaswa kuwa shuleni, na baadaye watazaa watoto ambao bado hawataweza kuwatunza vizuri.

Mara nyingi wazazi au walezi wa binti huamua kumfukuza nyumbani mtoto aliyepata mimba ikiwa ni namna ya kukimbia aibu au kumwadhibu dhidi ya alichotenda, lakini wanasahau kuwa walikuwa na wajibu wa kumlinda mtoto asitumbukie katika matatizo hayo.

Ikiwa mzazi au mlezi alishindwa kufuatilia maendeleo ya mwanaye kwa kipindi alichokuwa nyumbani ni wazi kuwa hakutimiza wajibu wake, naye ameshiriki kuzika ndoto ya binti ambaye huenda angekuwa daktari, rais, mbunge au injinia.

Hali hii inaonyesha jinsi ambavyo wazazi wamelegalega kwenye malezi ya watoto na kutoa nguvu kwenye kilio cha muda mrefu cha walimu kuwa jukumu la malezi limeachwa kwa walimu, jambo ambalo halipaswi kuwa hivyo.

Ni wakati sasa wa wazazi, walezi na jamii kubadilika kwa kuhakikisha wanakuwa karibu na watoto wao wote, hasa wa kike katika kipindi cha kuvunja ungo na kuzungumza nao namna gani watajitunza na kutojiingiza kwenye masuala ya kimapenzi au kuzuia matukio ya ubakaji na mengine ya udhalilishaji.

Wapo ambao wamebakwa na huenda wapo waliopata maradhi kwa kufanyiwa vitendo hivyo, kiasi cha kuwafanya kuwa na maumivu mara mbili ya kupewa mimba katika umri mdogo pamoja na mimba za utotoni na kukatisha ndoto za kielimu na kuambukizwa maradhi.

Kwa hali hii inadhihirisha kuwa bado asasi zisizo za kiraia na jamii kwa ujumla zinapaswa kuongeza bidii katika kufanya uraghibishi, kutoa elimu ya kujitambua kwa watoto wa kike na wazazi.

Tunatambua jitihada za serikali katika kupambana na mimba za utotoni na matukio ya ukatili kwa ujumla dhidi ya watoto, lakini isiachiwe yenyewe kwa kuona mtoto anapokwenda shule ni mali ya serikali, bali ni wajibu wa Asasi, wazazi na jamii kwa ujumla.

Katika hatua za ukuaji wa binadamu yeyote huhusisha mambo mengi na hukutana na mawakala wengi ambao humuwezesha kuwa na uzoefu wa mambo mengi kimaisha, na mojawapo ni kundi rika ambalo hukutana nalo mtaani kwake.


Tunaona kuna uwezekano mkubwa wa mtoto kukutana watoto wengine au watu wazima ambao watamshawishi kuingia kwenye matendo hayo.

Ndio maana kuna Tamko la kuwalinda watoto ambalo lilitolewa na Uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) (sasa Umoja wa Afrika -AU) kutokana na mauaji ya kikatili yaliyofanywa na serikali ya Makaburu Afrika Kusini mwaka 1976.

Ndio maana tamko hilo lilizaa Siku ya Mtoto wa Afrika, ambayo maadhimisho yake yalifanyika mapema wiki hii. Tuweke mkazo kwa wazazi na walezi kuwalinda watoto muda wote.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge

# Kutomaliza dozi, kujitibu famasi nazo vyanzo maradhi aina yake



Na Sabato Kasika

**KUNA** mtindo uliozoeleka kutoka kwa baadhi ya watu, watumiaji wa dawa hasa za kukabili bakteria, pasipo ushauri wa daktari.

Ni hali inayotajwa kuwa ya hatari, kwa vile mtumiaji anajiingiza katika hatari ya kujitengenezea sumu mwilini, pasipo kujijua.

Wataalamu wa afya wanasema, kanuni ya kutumia dawa kuna umuhimu wa umakini na nia bora ni kumhusisha mtaalamu wa afya, awape ushauri kwanza na sio uamuzi wa mgonjwa kusonga kununua dawa, bila ya ushauri nyuma yake.

Wataalamu wa afya, wanaorodhesha madhara aina sita, mtu anapotumia dawa bila ya kufuata ushauri wa daktari. Mojawapo ni kuongeza sumu mwilini, kwa vile dawa zimetengenezwa kwa kutumia kemikali, ambazo za mwongozo na mipaka.

Kunywa au kumeza dawa kwa mwongozo wa hisia na mantiki binafsi, kunasababisha utengenezaji usugu wa maradhi, unaozaa saratani na kuangukia kifo.

Dawa hiyo inapomezwa pasipo mwongozo na kanuni za kitaalamu, iko wazi zinaathiri afya ya mama na mtoto. Hiyo inafanya, kupata ushauri wa mtaaalamu wa afya mwenye dhamana ni muhimu.

Hapo ndipo inamwibua mtu kama vile mjamzito anatakiwa kuwa makini kutokana na hali yake, pale anapohitaji kutumia dawa za aina fulani, kwani inapofanyika kosa ni ajali inayogusa mbali, mtoto na mama tumboni.

Kwa maumbile ya mwanadamu, suala la watu kuugua maradhi mbalimbali ni kawaida. Shida kuu mojawapo ni, ama uvivu au kutopenda kufika hospitalini, kupata huduma za kiafya kama vile kufanyiwa vipimo au kupata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa madaktari.

Watu wanakimbilia katika mbadala wa kuwapo maduka ya dawa baridi, pale baadhi yao wanapojisikia kuumwa na wanajikuta wanatumia dawa hizo pasipo uchunguzi sahihi wa kiafya.

Hapo inaopaswa kuelewana, kwamba haimaanishi kuona matumizi ya dawa. La hasha! Ipo wazi dawa zimetengenezwa kutibu maradhi mahsusi, baada ya kubainika.

Wataalamu wa afya wameweka wazi, kwamba matumizi ya dawa bila kufanya uchunguzi wa kitaalamu, ni kikabidhi nafsi zetu jirani na hatari kubwa.

Kuna lingine sura ya pili. Kuna watu wanafuata kanuni na taratibu zote za kitabibu kupitia maelekezo ya kitaalamu na hatua zake, ila shida inagaukia katika kumalizia dozi za dawa wanazopewa na hasa pale wanapojisikia nafuu.

Ni mtazamo wa namna hiyo, watu wanaenda kupata huduma katika maduka ya dawa baridi, lakini dozi ya mtu mmoja wanagawana wawili, pale wanapokuwa na magonjwa yanayofanana.

Hapo kuna hasara mbili. Kwanza hakuna aliyepimwa na akagundulika au kuthibitika anachoumwa na kwa namna na kiasi gani, pili madhara ya kupata dozi chini ya kiwango kinachohitajiwa.

Katika juhudi zake za kuwapo mtindo huo hatari, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hivi sasa imeamua kuifanyia kazi kampeni kuwataka watu wamalize dozi wanayoandikiwa na madaktari.

Ni wajibu wa kila mmoja kufuatilia kinachotangazwa ya wizara, hasa msisitizo wa wagonjwa kumaliza dozi, ikiwamo katika hatari ya janga la malaria, kwani kutoimaliza ni kusababisha ugonjwa huo sugu.

Kinachotakiwa ni watu wajipe nafasi ya kufuatilia matangazo hayo ya serikali na kuyazingatia ili waachane na mtindo wa kutomaliza dozi au kugawana dawa, ambazo kwa ajili ya mgonjwa mmoja.

Upo ukweli, kinachotufikisha wanajamii katika ukweli huo mwingine ni uelewa mdogo wa baadhi ya watu kuhusu matumizi ya dawa kikamilifu au uzembe wa kutozingatia matumizi sahihi ya dawa kama wataalamu wa afya wanavyoelekeza.

Ninaamini, kinachosisitizwa ni kwamba wanafuatilia matangazo ya wizara na kile kinachosisitizwa na wataalamu wa afya ni cha msingi, iwapo kitazingatiwa na kufanyiwa kazi na kila mmoja.

Kimsingi, mgonjwa anatakiwa kuhakikisha anamaliza dozi aliyopewa, asithubutu kuacha kunywa dawa kabla ya kumaliza dozi yote kwa sababu tu anaendelea vizuri, ni hatari kwake.

# Samia, JK kushuhudia kuapishwa Rais Burundi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, leo anatarajiwa kuongoza ujumbe wa Tanzania nchini Burundi kwenye sherehe za kuapishwa kwa Rais Mteule wa nchi hiyo, Evariste Ndayishimiye.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, alisema hayo jijini Dar es Salaam katika Ubalozi wa Burundi nchini, alipokwenda kusaini kitabu cha maombolezo kufuatia kifo cha aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Pierre Nkurunziza kufariki dunia Juni 9 kwa maradhi ya moyo.

Alisema kutokana na uhusiano wa karibu baina ya nchi hizo mbili, Rais wa Tanzania Dk. John Magufuli ameamua kuongeza ujumbe wa Tanzania kwenda Burundi, unaoongozwa na Makamu wa Rais Samia ambaye ataambatana na Rais mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete.

Prof. Kabudi alisema kuwa hayati Nkurunziza amefanya kazi kubwa ya kuiunganisha Burundi na kuifanya nchi hiyo kuwa moja ya nchi zenye umoja na amani katika bara la Afrika, pia kuirejeshea matumaini na amani ya demokrasia na kudhihirika katika uchaguzi mkuu uliofanyika mwaka huu na kumalizika kwa amani.

Kwa upande wake Balozi wa Burundi nchini Tanzania, Gervais Abayeho, alisema ubalozi huo na Warundi kwa ujumla wamepokea kwa mshtuko na majonzi taarifa za kifo cha Rais Nkurunziza hasa baada ya kumalizika kwa uchaguzi, Rais huyo alikuwa akiendelea na shughuli zake kama kawaida ikiwa ni pamoja na kufanya mazoezi.

Alisema wakati wakiendelea na maombolezo ya kiongozi huyo, Warundi wote wanamshukuru Mungu kuwa tayari alikwishapatikana kiongozi mwingine ambaye ni Rais mteule na baada ya kuapishwa na kuwa rais mpya wa Burundi, shughuli nyingine na siku ya kufanyika kwa maziko ya Nkurunziza, zitafahamika.



Mkazi wa jijini Dar es Salaam akinawa kwenye bomba lililopasuka na kuvujisha maji katika eneo la Mabibo, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## DC alalamikiwa kuzuia maziko eneo la familia

**Na Faustine Feliciane**

MKUU wa Wilaya ya Misenyi mkoani Kagera, James Mwira, amelalamikiwa na wakazi wa kijiji cha Kashozi B, Kata ya Kassambya, wilayani humo kwa kuzia maziko na kufukia kaburi walilotaka kuzika.

Akizungumza kwenye ofisi za gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, mmoja wa wakazi hao Linus John, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi inawazuia wakazi wa eneo hilo kuzika ndugu zao kwenye maeneo na mashamba ya familia kwa madai kuwa maeneo hayo yapo kwenye ramani ya mipango miji.

"Hatupingani na serikali katika mchakato wa maendeleo, tunacholalamika ni kwamba hakuna maelekezo tuliyopewa ya kuzuiwa kuzika ndugu zetu kwenye maeneo yetu na wala hawatuambii maeneo mbadala, wazee wetu wamemiliki maeneo haya kwa miaka mingi na hata hiyo mipango miji imekuja kuwakuta, wanachofanya ni ubabe," alilalamika John, aliyefiwa na dada yake mwanzoni mwa mwezi huu na kuzuiwa kuzika.

Malalamiko hayo yameungwa mkono na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kashozi B, Rochius Bukambo, ambaye alisema kwa sasa watu wamekuwa na chuki na serikali yao ya wilaya kutokana na amri ya kuzuiwa kuzika katika maeneo yao.

"Wangefuta taratibu za kutuhamisha katika maeneo haya wanayosema yapo ndani ya mipango miji, kwa miaka mingi wakazi wa huku tumekuwa na kawaida ya kuzika ndugu zetu kwenye makaburi ya familia ambayo yapo kwenye maeneo ya familia, kutuzuia bila kutupa maeneo mbadala ni kutuonea," alilalamika Bukambo.

John akielezea mkasa wa kuzuiwa kumzika dada yake kuwa alifuata taratibu zote zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na kuomba kibali cha maziko kwenye makaburi ya familia yaliyopo ndani ya eneo lao, lakini alizuiwa dakika chache kabla ya kumzika dada yake.

"Wakati ibada ya mazishi ikiendelea mkuu wa wilaya alikuja na askari wakati tayari tukiwa tumechimba kaburi na kulijengea tukisubiri ibada kumalizika tuzike, pamoja na mazungumzo DC Mwira, aliwaamrisha mgambo wa kijiji kufukia kaburi na kuzuia, wakati anatoa maagizo hayo alikuwa ameondoka kimya kimya," alidai John.

Alisema kuwa iliwalazimu kwenda kuomba uongozi wa kanisa kuzika ndugu yao kwa kuwa mwili ulianza kuharibika.

"Hayo maeneo wanayotuzuia ndipo tulipozika ndugu zetu kuanzia mababu zetu na familia ilitenga kwa ajili hiyo, na huu ndio utaratibu wa watu wa Kagera, ndugu zao kuwazika kwenye makaburi ya familia, wanatuzuia bila kutupa mbadala wa makaburi yetu," alisema.

Akijibu malalamiko hayo, Mkuu wa wilaya hiyo James Mwira, alikiri kutokea kwa sakata hilo na kufafanua kuwa serikali haijayachukua maeneo hayo kama wanavyodai, bali maeneo hayo ni ya mipango miji ambayo tayari yametengwa.

"Ni utaratibu wa kawaida wa serikali, hatujayachakua wala hakuna mtu binafsi aliyeyachukua au kuwazuia kuzika, kanuni zipo na tumewataka wazisome."

"Wanapaswa kuomba kibali upya, lakini pia hawatakiwi kuyaendeleza maeneo hayo kwa namna yoyote, hakuna hila yoyote au labda DC anachuki, hapana ni utaratibu tu," alisema Mwira.

Naye Mkurugenzi wa Wilaya hiyo (DED), Innocent Mkandala, alisema maeneo hayo ni ya mipango miji.

## Vyama visivyo na uwakilishi vyakubali kanuni za uchaguzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VYAMA vya siasa vinavyolalamikia kulazimishwa kutia saini fomu za kanuni za maadili ya uchaguzi, vimetakiwa kuacha kutumia suala hilo kutafuta huruma wakati wa Uchaguzi Mkuu.

Rai hiyo ilitolewa jana na vyama vya siasa 12 ambavyo ni chama cha DP, NRA, AAFP, UDP, ADC, Makini, UMD, SAU, UPDP, NLD, TLP na CCK baada ya kukagua ujenzi wa jengo la Tume ya Uchaguzi nchini (NEC), jijini hapa.

Akizungumza baada ya kutembelea jengo la NEC, Katibu wa DP, Abdul Mluya, alisema baadhi ya wanasiasa wanadai kuwa walilazimishwa kusaini fomu jambo ambalo si kweli na kuvitaka kuacha kutumia hoja hiyo kama uchochoro wa kutafuta huruma ya Watanzania.

"Nimeanza kuona baadhi ya wanasiasa wakilalamika kabla ya kuingia uwanjani, hivi karibuni tulisaini maadili ya uchaguzi ambayo yaliandaliwa NEC kwa kushirikiana na vyama vya siasa, Tume ilituletea rasimu na sisi tukatoa maoni," alisema.

Alifafanua kuwa walisaini fomu yenye rasimu, maoni na majibu kuhusu mapendekezo ya chama yaliyokuwa yametolewa.

"Zile fomu tulisaini kwa haki kabisa, kwa utaratibu uliostahili kama mtu anatafuta uchochoro wa kutafuta huruma kwa wananchi kupitia kanuni hizi ni vyema asiingie katika uchaguzi ili atuache sisi wengine ambao tulikuwa tunakagua viti bungeni juzi (kuvunjwa kwa bunge)," alisema.

Naye, Katibu Mkuu wa Chama cha AAFP, Rashid Rai, alisema wana imani na Tume huku akiitaka ihakikishe inatenda haki ili isiwe chanzo cha vurugu.

"Uchaguzi huu hatutarajii kuonekana kuwa na tatizo lolote litakaloleta joto kwa sababu ya uchaguzi," alisema.

Alisema wanaamini kuwa Tume itaendelea kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria, Katiba ili kusitokee kitu chochote kitakachoharibu uchaguzi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa NRA, Hassan Almas, alisema wanaamini Tume na wanashangaa walikuwa wabunge katika Bunge la 11 wanavyoilalamikia.

Kuhusu jengo, katibu huyo alisema ziara yao ni ishara kuwa chombo hicho kinakubali kushauriana na vyama vya siasa.

Awali, akitoa maelezo ya jengo hilo, Mshauri Mwelekezi kutoka Chuo cha Ardhi, Godwin Maro alisema ujenzi wa jengo hilo limekamilika kwa asilimia kati ya 90 na 92.

Alisema jengo litakalotumika kama ukumbi wa kutangazia matokeo limekamilika kwa asilimia 75 na ujenzi unafanywa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

"Jengo litaanza kutumika Julai mwaka huu kwa ajili ya wagombea urais kuchukulia fomu za kuwania nafasi hiyo," alisema.

# Kibano chaja fedha za NGO

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameyataka mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) kubanwa katika matumizi ya fedha zinazotolewa na wafadhili ili kuwa na uwazi kwenye matumizi yake.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akizindua mwongozo wa uratibu wa mashirika hayo, uliofanyika jijini hapa.

Alisema baada ya kupitishwa kanuni za kusimamia mashirika hayo Desemba 2018, mashirika 115 yaliangaliwa ambapo hadi Mei 30, mwaka huu kuna Sh. trilioni 3.9 zimeingia kupitia mashirika hayo.

"Lazima tujue zimekwenda kufanya nini, kwa hiyo wenzetu wa Wizara ya Fedha tunafurahi mpo pamoja nasi, lakini tuendelee kuwabana wafadhili, hatusemi wasiwape, bahati nzuri na mimi nimetoka huko kwenye mashirika nimekaa miaka miwili, hatusemi watu wasipewe fedha ila tunataka kujua zinakwenda wapi," alisema.

Waziri Ummy alisema kinachotakiwa ni kujua fedha hizo zinakwenda wapi na zinaenda kufanya nini.

"Wala hata kama wakilipana mishahara mizuri haina shida ila nasisitiza lazima tuweke kipengele, kama unafanya kwenye elimu tunataka kuona kitu 'touchable' huko huko," alisema.

Hata hivyo, alisema changamoto ya kutokuwa na takwimu ni kutokuwapo na uwazi kwenye utendaji kazi wa mashirika.

"Mwongozo huu sasa utatusaidia katika kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika utendaji kazi wa mashirika na ufanisi katika maendeleo, tunachojifunza kuna fedha nyingi zilikuwa zinatumika kwenye mambo yasiyo na tija kwa wananchi," alisema.

Aliongeza: "Shirika linaweza kuwa limepata Sh. bilioni moja lakini mwisho wa siku lazima tumbane tujue inakwenda kutatua matatizo gani ya wananchi, huwezi ukawa na Sh. bilioni moja kazi ni kutoa matangazo, lakini haijasaidia kujenga zahanati wala kununua dawa."

Waziri huyo alisema lazima wabanwe kwa kuwa mtu hawezi kutumia Sh. bilioni moja kwenye matangazo ya televisheni lazima yaonyeshe namna yalivyosaidia wananchi.

"Nimefurahi sasa kila wizara itaingia hapa, sisemi wasitangaze, lakini lazima tuwabane unapotumia Sh. bilioni moja matangazo ya kila baada ya dakika 10 yamemsaidia vipi mama mjamzito, yamemsaidia vipi mtoto wa kike, lazima yatusaidie kujenga madarasa hata kama ni kazi ya serikali," alisema.

Kadhalika alisema takwimu za usajili wa mashirika hayo zinaonyesha kuwa mwaka 2015 mwezi Juni kulikuwa na mashirika 7,477, na yameongezeka hadi 10,446 mwezi Juni 2020, kati yake yakiwamo mashirika ya kimataifa, kitaifa na kimkoa.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, alisema mwongozo huo unaboresha mazingira ya utendaji kazi wa mashirika hayo ili yatoe mchango kwa Taifa.



Mkuu wa Jeshi la Polisi, Simon Sirro, na wasaidizi wake wakishiriki kwa njia ya mtandao mkutano wa Jumuiya ya Shirikisho la Wakuu wa Majeshi ya Polisi wa Nchi za Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SARPCCO) unaojumuisha nchi 15 ikiwamo katika mkutano wa kawaida wa kiutendaji, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JESHI LA POLISI**.

# Majaliwa aweka saini kitabu cha maombolezo kifo Nkurunziza

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, jana alitia saini kitabu cha maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Burundi, Pierre Nkurunziza na kutoa pole kwa wananchi wa nchi hiyo kwa niaba ya Rais John Magufuli.

"Kwa niaba ya Mheshimiwa Rais John Magufuli, nimekuja hapa kutoa pole na salamu za rambirambi kwa serikali na wananchi wa Burundi kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa nchi ya Burundi. Mheshimiwa Rais na Watanzania wote tumepokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa taarifa za kifo chake."

Waziri Mkuu ameyasema hayo akiwa katika Ofisi za Ubalozi wa Burundi, Upanga jijini Dar es Salaam baada ya kusaini kitabu cha maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Nkurunziza aliyefariki Juni 9, 2020 kutokana na mshtuko wa moyo.

Alisema Tanzania na Burundi ni nchi zenye historia ndefu na mshikamano wa muda mrefu, hivyo alitumia fursa hiyo kuwasihi wananchi wa Burundi wawe watulivu katika kipindi hiki cha majonzi. "Serikali ya Tanzania itaendelea kudumisha umoja na mshikamano kati yake na Burundi."

Awali, Balozi wa Burundi nchini, Balozi Abayeho Gervais, ametumia fursa hiyo kumshukuru Rais Magufuli kwa ushirikiano mkubwa anaoutoa kwa Taifa hilo na kwamba anatarajia umoja na mshikamano huo utadumu milele na milele.

"Tunamshukuru Rais wa Tanzania amepeleka ujumbe mkubwa Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan na Rais mstaafu wa Awamu ya Nne Dk. Jakaya Mrisho Kikwete nchini Burundi kwa ajili ya kushuhudia uapishwaji wa Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye ambaye anatarajiwa kuapishwa kesho Juni 18.

Akizungumzia kuhusu kifo cha aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Balozi Gervais alisema wamepokea kwa mshtuko mkubwa kwa sababu alikuwa bado ni kijana akiendelea kufanya shughuli zake. "Hii yote ni mipango ya Mwenyezi Mungu na sote tupo safarini."

# Watoto 80 wapatiwa bima ya afya

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

JUMLA ya watoto 80 wenye matatizo ya ubongo wanaolelewa katika kituo cha Amani kilichopo Chamwino, Manispaa ya Morogoro, wamepatiwa msaada wa bima ya afya kutoka kwa taasisi inayojishughulisha na biashara ya mitandao ya QNET.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Ester Mshaga, alisema lengo la kutoa msaada huo ni kurahisisha upatikanaji wa huduma za matibabu kwa watoto wenye tatizo hilo.

"Tumeamua kutoa msaada huu katika kituo hiki kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa huduma za matibabu kwa watoto hawa kwa kuwa suala la matunzo ni letu sote na siyo kituo tu hivyo wadau wengine nao wajitokeze kuunga mkono," alisema Ester.

Alisema, pia taasisi yake imetoa shilingi milioni moja ili ziweze kutumia kutatua changamoto kituoni hapo.

"Serikali yetu imekuwa ikionyesha kuwajali sana wanyonge hivyo na sisi leo tumeamua kuunga mkono juhudi hizo kwa kuwa watoto hawa nao pia ni wanyonge na bado tunaendelea kuwasaidia kwa hali na mali," alisema Ester.

Alisema watoto hao hawakupenda kuzaliwa hivyo bali ni mpango wa Mungu kwa hiyo Watanzania wana kila sababu ya kuonyesha matendo ya huruma kwa kuwafariji ili waweze kujiona wenye furaha kama watoto wengine nchini.

Aliipongeza uongozi wa kituo hicho kwa kuonyesha upendo wa hali ya juu kwa watoto hao malezi yenye mapenzi ya dhati.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Beatus Sewando, aliushukuru uongozi wa taasisi hiyo kwa kuwapatiwa msaada huo na ambao alisema utasaidia kutatua baadhi ya changamoto hususani ya matibabu.

Sewando aliwaomba wadau wengine kujitokea kusaidia kutatua changamoto hizo na kwamba malezi ya watoto hao ni magumu, lakini anamshukuru Mungu anawasaidia kubiliana nazo kila siku.

Aliwataka wazazi kuonyesha upendo wa dhati kwa watoto wao na siyo kuwatelekeza baada ya kuwafikisha kituoni hapo kwa kuwa kitendo hicho hakionyeshi picha nzuri kwa mtoto na kinamfanya ajione mpweke kila wakati.

# Maalim Seif ataka tume huru Oktoba

**Na Boniface Gideon,** TANGA

MWENYEKITI wa Chama cha Act-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, ameyachambua mambo matatu ambayo Rais John Magufuli hakuyatilia mkazo wakati akilihutubia Bunge kwa ajili ya kulivunja jijini Dodoma juzi.

Alisema pamoja na mambo mengi anayoyafanya Rais Magufuli, lakini kuna baadhi ya mambo yanaoneka hayapewi kipaumbele, huku akiyataja mambo hayo matatu kuwa ni tume huru ya uchaguzi, ugumu wa maisha kwa wananchi na haki kwa wananchi na wanaharakati.

Akizungumzia suala la tume huru ya uchaguzi, Seif alisema:

"Rais Magufuli amevunja Bunge, lakini kuna mambo amezungumza kwa kukimbia, hii inaonyesha kuwa hakuna uchaguzi huru na haki kwa kupitia tume iliyopo sasa hivi."

Aliongeza kuwa suala la ugumu wa maisha limekuwa kubwa kwa wananchi na kwamba alishangaa kuona Rais hajalizungumzia bungeni.

"Ugumu wa maisha ni mkubwa zaidi, lakini hilo hajalizungumzia kabisa sijui kwanini," alisema Seif.

Akizungumzia suala la haki, Maalim Seif alisema kumekuwapo na matukio mbalimbali nchini, na kwamba ni vyema Jeshi la Polisi na vyombo vya ulinzi na usalama kuacha tabia ya kujihusisha na siasa.

"Tunaona mataifa mengi duniani kama Uingereza na Marekani... majeshi yao yana misimamo, hayajihusishi na siasa hata Rais Trump alipotoa maagizo ya jeshi kuingilia kati ili kudhibiti maandamano, jeshi lao lilionyesha msimamo wake kwa kukataa kuwapiga raia wenzao," alisema Maalim Seif.

Katika hatua nyingine Maalim Seif ameendelea kuzibomoa ngome za Chama cha Wananchi (CUF) baada ya kupokea viongozi 176 na madiwani watano kutoka chama hicho mkoa wa Tanga.

Akizungumza na wanachama wa ACT-Wazalendo, Seif alisema Tanga ilikuwa ngome kubwa ya CUF, lakini kutokana na baadhi ya viongozi kuwa na tamaa walisababisha migogoro ya ndani.

"Binadamu ni dhaifu sana, unapewa heshima, lakini ukipewa kitu kidogo unasahau," alisema.




Mwenyekiti wa Chama cha Act-Wazalendo, Maalim Seif Hamad, akizungumza na wanachama wa chama hicho Mkoa wa Tanga juzi, wakati wa ziara yake ya siku moja. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Uchangiaji wa damu Ruvuma wafanikiwa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MRATIBU wa Damu Salama katika Mkoa wa Ruvuma, Imani Mbuzi, amelipongeza Shirika la Msalaba Mwekundu (Red Cross) Tanzania mkoani humo kwa kuhamasisha uchangiaji damu chupa 800.

Mbuzi alitoa pongezi hizo Siku ya Kilele cha Maadhimisho ya Uchangiaji wa Damu Kitaifa iliyoanza Juni tano hadi Juni 14, mwaka huu.

"Shabaha ilikuwa ni kila halmashauri kuchangia chupa 100 za damu na kufanya jumla ya chupa 800 katika halmashauri zote nane, kutokana na uhamasishaji mkubwa unaofanywa na Red Cross tutavuka lengo kwa sababu idadi ya watu wanaojitokeza ni kubwa," alisisitiza Mbuzi.

Alisema katika kituo cha hospitali ya rufani sasa zimekusanywa zaidi ya uniti 55 na kwamba idadi ya watu wanaojitokeza kuchangia imeongezeka kutoka watu wawili kwa siku hadi 12 kwa siku.

Kwa mujibu wa Mbuzi, Red Cross imefanyakazi kubwa ya kwenda kwenye mikusanyiko ya watu kama sokoni, nyumba za ibada, madereva wa pikipiki, barabarani kuhamasisha kuchangia damu hali ambayo imesababisha wengi kujitokeza.

Kwa mujibu wa Mbuzi, bila Red Cross uchangiaji wa damu mwaka huu ungekuwa na changamoto kubwa kutokana na janga la corona ambalo limesababisha kushindwa kuweka mahema sehemu za wazi na kutangaza ili watu wafike kuchangia.

Awali, Mwenyekiti wa Red Cross mkoa wa Ruvuma, Judith Kapinga, alisema wateja ambao wamehamasishwa wanafika kwenye vituo vya kuchangia damu.

Aidha, alisema mwitikio ni mkubwa licha ya kukabiliwa na changamoto za kuacha shughuli zao kwa muda na kufika kuchangia damu vituoni na kwamba Redcross imedhamiria kuvuka malengo ya uchangiaji damu ili kuwa na benki ya kutosha ya damu kwa ajili ya kuokoa maisha ya watanzania wanaohitaji damu.

"Wahitaji wa damu ni wengi wakiwamo wajawazito, watoto chini ya miaka mitano, watu waliopata ajali, watu waliozaliwa na seli nundu na watu wanaofanyiwa upasuaji, hawa wote ni waathirika wa damu," alisisitiza.

**Shabaha ilikuwa ni kila halmashauri kuchangia chupa 100 za damu na kufanya jumla ya chupa 800 katika halmashauri zote nane, kutokana na uhamasishaji mkubwa unaofanywa na Red Cross tutavuka lengo kwa sababu idadi ya watu wanaojitokeza ni kubwa**

# Taasisi yapania kuzalisha maofisa tabibu mahiri

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Sayansi na Technolojia ya Vignan (VIST), imeahidi kuwanoa maofisa tabibu wengi zaidi na wenye weledi na maadili ili kuongezea nguvu jitihada za serikali za kuwekeza kwenye sekta ya afya.

Imesema serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa kwenye sekta ya afya, hivyo wadau binafsi wanawajibika nao kuweka nguvu zao ili kuongeza wataalamu wengi kwenye sekta ya afya.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Naidu Katuri kuhusu uzinduzi wa taasisi hiyo pamoja na masuala mbalimbali kwenye sekta ya afya.

Alisema kwa kuwa kuna uhaba wa watumishi wa sekta ya afya hususan maofisa tatibu, taasisi hiyo imejipanga kuhakikisha inazalisha wataalamu hao wengi na wenye sifa.

Alisema taasisi yake imegundua wataalamu hao wanahitajika zaidi maeneo ya vijijini ambako ndiko idadi kubwa ya Watanzania iliko.

Katuri alisema taasisi hiyo, imejizatiti kufanikisha maono ya mwaka 2025 ya mkakati wa kitaifa wa kukukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini.

Alisema VIST itatumia wahadhiri wake wenye uzoefu wa kutosha na vifaa vya kisasa vya kufundishia kuhakikisha wanatoa wataalamu walioiva watakaokwenda kufanya kazi kwa maadili na weledi.

"Tumeshapewa baraka na Baraza la Taifa Ithibati (NACTE) na limeanza kupokea maombi ya wanaotaka kujiunga na stashahada ya tiba ya (NTA Level 4-6) kwa mwaka wa masomo wa 2020-21," alisema.

Aidha, alisema wanatarajia kwa kuanza wawe na wanafunzi 150 wa stashahada ya tiba na mpaka kufikia mwaka ujao wa masomo wawe na wanafunzi zaidi ya 1,000 kwenye fani mbalimbali.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Tellack, akizungumza na wakulima wa tumbaku, Halmashauri za Ushetu na Bukombe mkoani Geita alipotembelea masoko ya zao hilo, katika moja ya ghala la tumbaku la Kampuni ya Alliance One Busoka. Wa pili kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Taasisi kutoa mkopo wa bil.40/- kwa walioajiriwa

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Huduma za Kibenki ya Faidika, imetenga zaidi ya Sh. bilioni 40 kwa ajili ya kuwakopesha Watanzania wenye ajira kupitia programu ya 'Mshahara Wako, Mkopo Wako'.

Mkurugenzi Mkuu wa Faidika, Baraka Munisi, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa mikopo hiyo inatolewa ndani ya saa 24, endapo mkopaji atatimiza masharti yaliyowekwa.

Munisi alisema kuwa wameamua kutenga kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kuboresha maisha ya Watanzania.

Sambamba na hilo, alisema wameongeza kiwango na muda wa malipo ambapo kwa sasa wanatoa mikopo kuanzia Sh. 200,000 mpaka Sh. milioni 70 na malipo yake yanatakiwa kufanyika kwa kipindi cha miezi sita hadi 84.

Alisema kuwa mbali ya kuongeza kiwango cha kukopa na muda wa mkopaji kulipa deni, pia wamepunguza riba ambayo inatoa nafuu kwa mkopaji kulipa deni lake.

Alifafanua kuwa mikopo hiyo inakuwa inatolewa kupitia matawi yao 16 na ofisi zaidi ya 88 zilizopo nchini.

"Pamoja na changamoto za miundombinu, Faidika inaamini kuwa kila mtu anastahili kupata huduma ya kifedha ndiyo maana tumepanua wigo kupitia mifumo ya kisasa zaidi ya teknolojia ili kuwafikia Watanzania wote kwa lengo la kuboresha maisha yao," alisema.

Munisi alisema kuwa wafanyakazi wa serikalini na taasisi zilizothibitishwa, wanaruhusiwa kupata mikopo hiyo.

"Unachotakiwa kuleta ili kujipatia mkopo wako ni kitambulisho cha kazi, picha moja ya pasipoti, stakabadhi moja ya mshahara (salary slip) ya mwezi uliotangulia na taarifa za akaunti ya benki kuanzia miezi miwili na kuendelea. Faidika ina huduma za kipekee, rahisi, sahihi, nafuu za zenye kukidhi mahitaji," alitamba.

Alisema kuwa kwa wateja waliokopa wanaweza kutumia mikopo hiyo katika kuboresha maisha yao kupitia uwekezaji kwenye elimu, afya na kilimo.

Kwa mujibu wa Munisi, mikopo hiyo hufutwa pindi mdaiwa anapofariki dunia na taasisi yao itatoa rambirambi ya Sh. 200,000 kwa mfiwa.

"Taasisi yetu imedhamiria kuboresha zaidi maisha ya Watanzania kwa mwaka 2020 na kuendelea. Tunawaomba wananchi kuchangamkia huduma hii ambayo ni ya kipekee na rahisi," alisisitiza.

# TAMA: Corona iliathiri baadhi watoa huduma tiba kisaikolojia

**Na Happy Severine,** SIMIYU

CHAMA cha Wakunga Tanzania (TAMA) kimesema baadhi ya watoa huduma wakiwamo wakunga ambao walikuwa mstari wa mbele kuwahudumia wagonjwa waligundulika kuwa na ugonjwa wa corona, wamepata tatizo la kisaikolojia.

Chama hicho kimesema tatizo hilo lilisababishwa na hofu kubwa iliyokuwapo juu ya ugonjwa huo, ambayo ililetwa kwa kusambaa taarifa nyingi zenye ukweli na ambazo hazina ukweli katika mitandao ya kijamii na mitaani.

Hayo yamesemwa jana na Mratibu wa chama hicho, Martha Limoi, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya mafunzo ya siku mbili kwa watoa huduma mkoani humo ambayo yalilenga kuwaondolea hofu juu ya ugonjwa huo.

Limoi alisema watoa huduma wengi walipokuwa wakisoma kwenye mitandao ya kijamii na kusikiliza vyombo vya habari, huku wakiona idadi kubwa ya watu wakipoteza maisha kwenye nchi za Ulaya wengi waliingiwa na hofu.

Alisema chama chake kimebaini uwapo wa baadhi ya watoa huduma ambao walikuwa na woga wa jinsi gani wataweza kuwahudumia wagonjwa, wakati na wao wana familia na zinawategemea.

Alisema hata baadhi ya watoa huduma waliwakimbia wagonjwa kutokana na woga, kwani wengi wao walikuwa hawajui hatima ya maisha yao, huku wakitakiwa kwenda kupambana na ugonjwa huo.

"Wapo baadhi walifikia hatua ya kuona taaluma ya afya ni mbaya, kwanini walisomea, waliona taaluma hii kama mateso na kifo kwao, baadhi walitaka kuacha kazi, wengi walitengwa na familia zao na jamii," alisema Limoi.

Alisema watoa huduma hao licha ya kufuata miongozi yote ya kujikinga na ugonjwa huo, lakini bado walikuwa na hofu huku wakiwa hawajui hatima ya maisha yao na familia zao kwani walikuwa na woga mwingi.

"Hali hii imesababisha wengine kupata shida ya kisaikolojia kutokana na kukumbwa na msongo wa mawazo, walikuwa wakifikiria vitu vingi mpaka wanachanganyikiwa, lakini bado walitakiwa kwenda kazini kupambana," alisema Limoi.

Hata hivyo, alisema kuwa hotuba ambazo zilitolewa na Rais John Magufuli wakati wa ugonjwa huo ukishika kasi, zilibadilisha hali za watoa huduma na wengi walitokwa na hofu kubwa waliyokuwanayo.

"Tunamshukuru sana Rais Magufuli bila yeye hali ingelikuwa mbaya zaidi, hotuba zake zile ziliwaondoa hofu watoa huduma wote na wengi wakaanza kufanya kazi na kujiamini," alisema Limoi.

Mmoja wa wauguzi kutoka wilayani Maswa, Sigira Mkwende, alikiri uwapo wa hali hiyo, ambapo hata kwake ilitokea hasa hofu na mawazo mengi, huku akifikia uamuzi na kutaka kuacha kazi.

Alisema changamoto zaidi ni pale jamii na familia yake kumtenga, licha ya kutogundulika kuwa na ugonjwa huo ingawa alimhudumia mgonjwa mwenye ugonjwa huo.

"Tulikuwa na hofu kubwa na woga wa ugonjwa huu, nilifika hatua ya kutaka kuacha kazi na kuiona kama kazi ambayo inataka kunipelekea kwenye kifo, wengi hatukuwa na maandalizi ya ugonjwa huu, ndiyo maana tumepata tatizo la kisaikolojia," alisema Mkwende.

# DC aahidi kuwapa fedha watakaofaulu kidato cha 6

**Na Hamisi Nasiri, MTWARA**

MKUU wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, ameahidi kutoa zawadi ya Sh. milioni moja kwa kila mwanafunzi atakayefaulu kwa kupata wastani wa daraja la kwanza pointi tatu kwa shule za serikali zilizopo Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

Amesema lengo ni kutaka kuona kila mwanafunzi anafanya vvema katika mitihani ya kidato cha sita inayotarajia kufanyika hivi karibuni.

Kyobya alitoa ahadi hiyo jana mkoani Mtwara alipotembelea Shule ya Sekondari ya Wasichana Mtwara na Mtwara Ufundi kwa ajili ya kuwapa hamasa wanafunzi wa shule hizo kuelekea kwenye mitihani yao ya kuhitimu elimu ya sekondari.

Alisema ili kuhakikisha shule zote za sekondari za serikali mkoa wa Mtwara hasa ambazo zinaelekea katika kufanya mitihani yao ya kidato cha sita, ameona ni bora awatie hamasa wanafunzi kwa kutoa ahadi hiyo ya fedha kwa yeyote atakayefanya vizuri.

Aidha, Kyobya alisema pamoja na zawadi kwa wanafunzi pia ameahidi kutoa zawadi ya Sh. 500,000 kwa mwalimu atakayefaulisha kwa wastani wa daraja 'A' katika kila somo ikiwa ni sehemu ya kuwapa motisha walimu kufanya kazi kwa bidii.

Kyobya alisema ahadi hizo zote kwa wanafunzi pamoja na walimu zinalenga kuona mkoa wa Mtwara unafanya vizuri kitaaluma na kwamba wanafunzi wanafaulu vizuri na walimu wanafaulisha vizuri.

ama


ALHAMISI JUNI 18, 2020

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Mimba na ukatili ni mambo yaliyoshamiri kipindi corona**



Ukurasa 13

Ndivyo yalivyo maambukizi mkojo 'UTI' matibabu yake



Ukurasa 14

**Wenye ualbino wanaumizwa na mahitaji, kuchelewa matibabu**

AFYA

# Safari corona inapong'olewa kwa nguvu 'Neno la Muumba'

**Na Christina Haule, Morogoro**

JUZI Rais Dk. John Magufuli alipofunga rasmi Bunge alitamka kupungua kwa kiasi kikubwa athari za corona na akawatangazia Watanzania kurejea ruksa ya awali ya shughuli zao kama kawaida, ila akiwatahadharisha waendeleze umakini wa zama za janga hilo.

Hapo inapokelewa kwa hoihoi ya wanafunzi wa shule kurudi darasani aliyoitangaza Rais juzi, kufuata nyayo za dada na kaka zao wa vyuoni na shule za sekondari kidato cha sita waliokwishaanza.

Ni hatua inayofikiwa ndani ya jitihada ya miezi mitatu ya misukosuko kwa umma kwa ujumla. Mwenyezi alihusishwa kwa kiasi kikubwa, ikiwamo sala za kitaifa za siku tatu, hali ilioyoungwa mkono sana na umma wa waumini.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipozungumza katika nyumba ya ibada jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO.**

Inafahamika nyumba za ibada ni sehemu ya maeneo nyeti kijamii kitaifa iliyokabiliwa na msukosuko huo, hata watu wakaabudu katika utaratibu uliorekebishwa katika baadhi ya sehemu.

Nje ya nchi, mfano wa Korea Kusini, kanisa moja lilikumbwa na msukosuko, mkusanyiko wake uligeuka kitovu cha kuenea maradhi, waumini walipokutana.

Kuna nchi nazo ziliangukia na hata baadhi mpaka sasa, wako katika karantini za ndani baina ya maeneo na hata mikoa ya ndani. Ni ushuhuda wa corona sio salama!

Pengine leo hii kugeuza jamii ilikotoka nchini, kuna madoa ya maumivu ya baadhi ya misukumo ya virusi vya Covid 19 vimeshaacha vidonda nchini.

Kibinadamu, kuna lugha ya faraja inayobeba ukweli wa aina hiyo, ikitamka "yaliyopita si ndwele, tugange yajayo" na "maisha lazima yaendelee" kama alivyogusia Rais juzi Bungeni.

Hivyo, Tanzania inavyofungua mlango, hata ndege zinazowaleta watalii kuingia nchini na mikusanyiko kama ya soka viwanjani imerejea, ni hatua mpya kubwa.

Saudi Arabia, moja ya nchi inayoshikilila nguzo ya kiimani kwa watu duniani kwenda kuhiji huko, ilisimamisha kwa muda kutokana corona. Ni kipindi hamasa hiyo inawarejea waendaji kutimiza safari hiyo nyeti kiimani,

Alhaji Omari Kijangwa, muumini na mwandishi wa kitabu kinachouzwa ndani na nje, anayejitambulisha alishaenda Hijja mwaka 2007, bado anawekeza nguvu kubwa katika maombi dhidi ya corona, kwamba ni silaha ya kwanza kufungua milango yote, ikiwamo kwenye milango ya kuhiji.

Anafafanua maradhi ikiwemo ugonjwa ni sehemu ya mitihani unaosababisha maumivu kwenye miili ya watu na hata wengine kufariki.

Katika hilo, anasema Watanzania wanayo haki ya kushukuru kuwa na kiongozi wa nchi mwenye hofu ya Mungu, akiwasifu Rais Dk. John Magufuli na wasaidizi wake waandamizi ngazi ya taifa.

Hilo lilirejewa na Rais Dk. Magufuli, juzi bungeni alipomtamka Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, pamoja na Waziri mwenye dhamana na Afya, Ummy Mwalimu kwamba waliwajibika.

Alhaji Kijangwa, anawarejesha sifa viongozi nchini walivyowakusanya viongozi wa dini zote kumuomba Mungu kuwaondolea adha ya ugonjwa corona na daima hawakuweka zuio la makazi, jambo analolisifu, akitamka imeonyesha matokeo chanya katika kupunguza kasi ya kusambaa kwake.

"Kirusi cha Corona ni dhaifu kwa dua na maombezi mbalimbali. Yanatosha kukifukuzia mbali kikaondoka kwenye jamii yetu dunia nzima," anatamka, huku akishangilia kutofungwa nyumba za ibada.

Alhaji Kijangwa anaendelea:"Tutumie subira na imani, kwani ni silaha tosha kwa muumini wa kweli....zipo ibada zingine hazitakiwi kufanyika nyumbani."

Rais Dk. Magufuli alipozungumza na viongozi wa dini, aliwapa nafasi rasmi ya siku tatu, wasali na waumini wa dini zote, ikiwamo kufunga katika vita ya kiimani dhidi ya maradhi ya corona nchini.

Pia, waumini walishachukua hatua kama hiyo ya kumshukuru Mungu, kwa mwelekeo chanya wa msukumo huo wa kiimani na waendelea.

Katibu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Dk. Mecka Ogunde, anaelekeza shukurani kwa Mungu kwa mwekekeo wa majibu ya maombi ya kukabili janga la ugonjwa Corona.

Pia, alipozungumza kwenye Swala ya Eid Elfitri jijini Dodoma zaidi ya mwezi mmoja ulipoita, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alitoa taarifa zenye takwimu za unafuu wa maradhi kusambaa mwezi u.

Rais Dk. Magufuli kupitia hotuba zake za kuwajuza wananchi kuhusu vita ya corona, alidumu katika kutowawekea Watanzania mazingira ya kukabili ugonjwa yanayokinzana na maendeleo ya uchumi nchini, hoja aliyodumisha hadi juzi alipotangaza mageuzi makubwa ya kufungua milango.

Takwimu za mwisho za serikali, ambazo Waziri Ummy Mwalimu, alitaja ni kuwapo wagonjwa wanne kitaifa, wote jijini Dar es Salaam na zaidi vituo vingi vya karantini vilibaki vitupu.

Wakati mwelekeo wa uchumi unatarajiwa kupiga hatua kwa chanya ndani ya msukosuko wa corona duniani, Tanzania inatarajiwa ukuaji uchumi chanya kinyume na nchi nyingi kuangukia hasi, kwa mujibu wa uwasilisho wa wiki iliyopita kwenye Bunge la Bajeti la 'lala salama'.

AFYA

# Mimba na ukatili ni mambo yaliyoshamiri kipindi corona

## • SAUT yabuni dawati; RC, wadau wanena yao



Jerryness Jackson, mwanaharakati wa kijamii kutoka shirika la Hakizetu Tanzania, akitoa elimu ya kujikinga dhidi ya ukatili kijinsia kwa wakazi wa mtaa wa Mchongomani, jijini Mwanza. **PICHA: NEEMA EMMANUEL.**

**Na Neema Emmanuel,**

**MWANZA**

UGONJWA wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona ya (Covid -19), umetajwa kuwa changamoto kwa sekta ukatili wa kijinsia na hasa dhidi ya kinamama.

Kwanini? Jibu ni kwamba inatokana na wanafamilia kutumia muda mrefu wakiwa pamoja, ikitajwa inaibuka katika sura ya pili kuongezeka ukatili wa kijinsia.

Ni katika orodha hiyo kuwa changamoto ya ukatili wa kijinsia kingono na hasa mabinti, kutokana na ukweli kwamba hawapo shuleni kwa muda na wanatarajiwa kurejea masomoni siku 11 zijazo.

Hivyo, miezi mitatu ya maisha tofauti na waalivyozoea, imebainika kuwapo kundi la watoto walioingiza kwenye vitendo vya ngono tena 'zembe', jambo linalohatarisha kuongezeko mimba za utotoni na hata , magonjwa ya zinaa, ikiwamo Ukimwi.

**MDAU ANAELEZA**

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake, katika Siku ya Maadhimisho ya Afya ya Wanawake Duniani Mei 28, Mkurugenzi wa Miradi wa Shirika la Kutetea Wanawake na Wasichana la Haki Zetu, Gervas Evodius, anaorodhesha changamoto za corona.

Pia, anasema watu wamejikita zaidi kupambana na ugonjwa huo, huku wakisahau upande mwingine wa afya, ama mimba za utotoni au zisizisotarajiwa zenye kawaida ya kuendana na matukio kama watoto kutupwa baadaye, pia ukatili wa kibinadamu.

> **"Tunatakiwa kufahamu kwamba ukatili wa kijinsia unaathiri familia nzima na jamii nzima kwa ujumla, kwa hiyo ni vita ambayo sote tunatakiwa kushiriki katika kuvitokomeza," anasema Evodius.**

Anasema wasichana na wavulana, wanahitaji usimamizi thabiti kutoka kwa wazazi wawili na jamii, pia ulinzi dhidi ya ukatili, ikiwa ni wakati muafaka wa kuzungumza nao njia bora za kujikinga na ngono mapema, wakipatiwa elimu zaidi ya afya ya uzazi na makuzi.

Evodoius anahimiza wakati ambao watoto hawapo shuleni, wazazi wanapaswa kutumia fursa ya ukaribu nao, wakijadili mabadiliko ya miili yao, hedhi salama ikaoanishwa na uelewa wa kuwapo Wiki ya Hedhi Salama, ambayo nayo imeshapita.

Katika hilo anasisitiza kinababa ambao baadhi yao ni adimu majumbani, wawe na muda wa kutosha kuongeza mapenzi kwa wenza wao na sio kuendeleza ukatili.

"Tunatakiwa kufahamu kwamba ukatili wa kijinsia unaathiri familia nzima na jamii nzima kwa ujumla, kwa hiyo ni vita ambayo sote tunatakiwa kushiriki katika kuvitokomeza," anasema Evodius.

**CHUO KIKUU SAUT**

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mt. Agustino (SAUT), jijini Mwanza, Balozi Prof. Costa Ricky Mahalu, akifungua 'Dawati la Changamoto za Kijamii' chuoni hapo alikumbusha unyanyasaji wa aina yoyote.

Kwa mujibu wa Prof. Mahalu, ukiukwaji wa haki za binadamu ulishatamkwa na Umoja wa Mataifa mwaka 1948, kwamba binadamu wote wamezaliwa wakiwa uhuru sawa, katika masuala ya utu na haki.

Mtaalamu huyo anasisitiza kukabili unyanyasaji na uhusiano wake na ulinzi wa haki za binadamu, jambo ambalo mataifa duniani yako mstari wa mbele kuyatatua, ili kuwaletea haki na usawa wananchi wote.

Uamuzi wa chuo kikuu hicho kuanzisha dawati, unaelezwa unalenga kugusa changamoto nyingi za kijamii. Hapo zinaorodheshwa;unyanyasaji kingono, mabavu, kisaikolojia na kijinsia .

**RC & WADAU**

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, anakiasa Chuo Kikuu cha SAUT litumie dawati kuleta amani na vitendo vya ukatili visitumike kama mahakama.

Pia, anazungumzia suala la afya, akifafanua kwamba wamekuwa wabia na taasisi anayoitaja ya Aga Khan Develop Network na kunafanikisha majengo 28 ya vituo vya afya sehemu mbalimbali nchini, kumhuduma mama na mtoto.

Mdau wa harakati hizo, Simoni Chemu, anasema ni wakati muafaka familia zikaungana kiimani, ili kupata uponyaji unaowapa mapungfu ya kijamii yaliyotajwa, pia kuwarejesha amani wawe nje ya maovu.

Ni mawazo yanayoungwa mkono na mdau mwenza, Husna Kambarage, anayesema, jamii inapaswa kuungana kupinga yanayovunja amani hasa katika malezi, ili kupata mbadala wa upendo unaoelimisha watoto afya ya kujitambua na kuwajengea maarifa .

**MTAALAMU & MCHUNGAJI**

Lugodisha George, Mtaalamu na Muwezeshaji wa Huduma za Afya ya Uzazi wa Kujitegemea, anautaja ukatili ulivvyo ni pale binti anapata ujauzito, fursa zake nyumbani zinapotea ana anangukia changamoto kama kufukuzwa shule na nyumbani.

Ni hali mtaalamu huyo anayoeleza inaendana na hali kama ya kukimbiwa na mwanaume aliyempatia ujauzito, jamii inamtenga, binti anahamia mtaani anakoshidwa kupahimili, akiangukia athari kama kujifungua mtaani, kutoa mimba au kuwa kahaba.

Anataja chanzo kikuu, ni kwamba kasoro ya wazazi wanaposhindwa kuwa karibu kuwaandaa watoto, hawawapi elimu sahihi kuhusu maisha, hawapunguzi kuwanyanyasa au kuwajengea uwezo wa kimaendeleo.

"Hakika afya ya uzazi imepunguza maambukizi ya magonjwa mbalimbali pamoja na kushamiri kwa utoaji wa mimba mitaani," anasema George

Mwenyekiti wa Umoja wa Makanisa Mwanza, ambaye ni Askofu wa Kanisa la African Inland Church Tanzania (AICT), jijini Mwanza, Philipo Mafuja, anawaelekezea nasaha Watanzania kuomba waondolewe janga la kirusi Covid - 19, inayoendana na majanga kama kushuka uchumi na ukatili katika jamii.

Anakiri harakati za kujilinda na kujiepusha, kupitia imani za kidini umma unapaswa kubadilika na kuchukua tahadhari za kupambana.

Juzi katika hotuba ya kulivunja Bunge jijini Dodoma, Rais Dk. John Magufuli, alirejea kuwashukuru viongozi wa dini, kwa mchango wao wa kiimani, katika kupiga vita maradhi ya corona.



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha SAUT, Mwanza, Profesa Costa Mahalu. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# Ndivyo yalivyo maambukizi mkojo 'UTI' matibabu yake

**Na Jackson Paulo**

UGONJWA wa maambukizi ya njia ya mkojo au 'UTI' una kawaida, uwezekano wake kutokea ni katika sehemu yoyote ya mfumo wa mkojo.

Hapo inamaanisha, viungo kama vile kibofu mkojo, ureta (mrija unaoungana na kibofu), figo, na urethra (mrija unaunganisha kobofu na sehemu ya nje). Mara nyingi, wanawake wapo kwenye hatari kubwa zaidi ya kuugua maradhi ya UTI kuliko wanaume.

Hata hivyo, ikiwa 'UTI' itasambaa hadi kufika kwenye figo, hali ya mgonjwa huweza kuwa mbaya na hatari zaidi.

Kwa kawaida, madaktari hutibu maambukizi kwa njia ya mkojo wakitumia dawa za tiba ya bakteria, maarufu 'antibiotics.'

Hata hivyo, zipo njia kadhaa zinaweza kufuatwa na kupunguza uwezekano wa kupata maambukizo ya njia ya mkojo.

**DALILI UTI**

Baada ya mtu kupata maambukizo ya njia ya mkojo, huwa anaonyesha unaweza kupata kati ya dalili zifuatazo: Kuhisi kukojoa kila mara, kujihisi 'kuwaka moto' wakati wa haja ndogo; kutoa mkojo wenye rangi ya ukungu na harufu kali.

Mengine kwa mujibu wa wataalamu, maumivu ya nyonga (wanawake) kutoa mkojo wenye damu au mwekundu, homa na kujiskia uchovu.

Ni maambukizi yanayoanzia katika sehemu ya mwili inayotumika kuhudumia haja ndogo kwenda nje ya mwili, hali inayoanza baada ya bakteria kugusana na mlango kwa njia ya mkojo na kuanza kuzaliana kwenye kibofu.

Chanzo kikubwa cha 'UTI' ni bakteria ajulikanaye kwa jina la 'E. coli'. Kwa kawaida anaishi tumboni mwa binadamu na kuna wakati anasogezwa kutoka sehemu ya haja kubwa hadi ndogo.

Katika hilo zipo sababu kuu mbili; kusogezwa bakteria kwenda kwenye njia ya mkojo na namna ya kujisafisha, mara baada ya haja kubwa kwa kinamama, sambamba na kushiriki mapenzi.

Huwa, mara baada ya bakteria kugusana na sehemu ya haja ndogo, huwa inasafiri na kupanda hadi kwenye kibofu anakokaa, wanazalia na kusababisha maambukizi zaidi.

Kuna kawaida, maambukizo yanapoendelea, bakteria nao wanaelekea sehemu ya juu zaidi kwenye figo ambako wakifika, wanasababisha madhara yenye hatari za athari kubwa, iwapo matibabu sahihi hayatafanyika.

Pia, kuna mambo yanayochangia kuongezeka madhara hayo. Mosi, ni muundo wa kimaumbile, wanawake wote wapo katika hatari ya kuugua 'UTI' kwa sababu ya asili ya kimaumbile ambayo ni ukaribu mkubwa kati ya sehemu ya haja kubwa na ndogo.

Pia, wanawake huwa na mrija wa kutolea mkojo ulio mfupi kuliko wanaume. Hiyo inawapunguza umbali wa safari ya bakteria, wanaofanikiwa kufikia haraka zaidi kwenye kibofu cha mkojo na kuishia madhara.

Pili, kuna suala la ushiriki katika mapenzi; Wanawake kila mara wamekuwa wanataabika na maambukizo hupata 'UTI' zaidi, kuliko wasiofanya hivyo.

Kushiriki mapenzi kwa mwanamume zaidi ya mmoja kunaongeza uwezekano wa kupata 'UTI'. Hata hivyo kwenda haja ndogo kila baada ya tendo hupunguza uwezekano wa kupata maambukizi.

Tatu, maradhi hayo yanaziba mikojo, hasa pale mtu anapobanwa kwa mrija wa kutoa mkojo, inayozaa ama kama tatizo la mawe ya figo au tezi dume huwa katika hatari ya kupata 'UTI.' Ni hali inayosababisha kukwama mkojo, unaoongeza uwezekano wa bakteria kuzaliana.

Nne, matumizi ya mrija wa kusaidia kutoa mkojo 'catheter': Watu wanaotumia mrija maalum 'catheter' kwa ajili ya kusaidia kukojoa wapo katika hatari zaidi ya kupata 'UTI'.

Kuna la tano; upungufu wa kinga mwilini. Wenye kinga za chini mwilini, ni hali inayowaweka jirani na hatari ya kupata maradhi ya 'UTI.'


Hao ni pamoja na wenye maradhi ya Ukimwi, kisukari na walio katika matibabu yanayohusika na kupunguza kinga ya mwili kama vile kansa.

Sita, inagusa namna ya kinamama hao wanavyojisafisha, baada ya kupata haja kubwa. Iwapo mtu atafanya kutokea nyuma kwenda mbele, hapo kuna uwezekano mkubwa wa kupatwa na 'UTI'kwa sababu ya uwezekano wa kusogeza bakteria kutoka njia sehemu ya haja kubwa, kwenda ndogo.

Inashauriwa kwamba namna bora ya kujisafisha baada ya haja kubwa kwa mwanamke, ni kutoka mbele kwenda nyuma.



Huduma ya kupima mkojo ikiendelea. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Sampuri za mikojo zikisubiri kufanyiwa vipimo.



Ulivyo mkojo mchafu unaomtesa mgonjwa.

**AINA ZA UTI**

Zipo aina tatu za 'UTI' kulinga na sehemu ya mwili iliyoathirika ambazo ni, maambukizi

Kwenye figo 'pyelonephritis': ambayo ina dalili za maumivu katika sehemu za pembeni na nyuma ya nyonga, homa kali, kichefuchefu na kutapika

Lingine ni maambukizi kwenye kibofu, dalili zake huwa ni pamoja na kujisikia vibaya maumivu chini ya tumbo, kukojoa kila mara na kupata maumivu wakati wa haja ndogo, ikiambatana na mwonekano wa damu.

Kwenye mrija wa mkojo (urethritis)'; dalili yake kuu ni kujisikia kuwaka moto wakati wa haja ndogo.

**MADHARA YALIYOPO**

Mtu anapougua 'UTI' hata ana inapotibiwa, ni mara chache wanapatwa na madhara makubwa, lakini isipotibiwa, inamsababishia madhara makubwa kama kuharibika kabisa figo na maradhi mkojo mchafu kujirudia kila wakati.

Vivyo hivyo, anayeumwa akiwa mjawazito, kuna uwezekano wa kujifungua mtoto mwenye uzito pungufu au njiti, huku wanaume nao njia zao za mkojo zinapungua upana kwenye mrija nafigo inashindwa kufanya kazi yake, au hata kifo kuwakuta.

**MATIBABU**

Namna ya kutibabu inategemea hali ya mgonjwa, kama vile kwenye umri, jinsia, kiwango bakteria walivyosambaa na ujauzito ulivyo.

**KUIKABILI**

Maana yake ni mgonjwa ama kuwahi au kuwahishwa penye matibabu rasmi ya kihospitali ambako tiba kama kwa mwenye ama 'UTI' isiyo kalia au kwenye kibofu au mrija wa mkojo, huwa anatibiwa kwa kumeza tu dawa za bacteria -antibaiotics.'

Kwa wenye'UTI' iliyosababishwa na vijidudu vinavyosababisha magonjwa ya zinaa yaani 'STD' huhitaji matumizi ya dawa zaidi ya aina moja. Hata hivyo, wajawazito na watoto hawapaswi kutumia baadhi ya dawa kutokana na madhara yanayoweza kuwatokea.

Ili kujiepusha na maradhi hayo, mgonjwa anatakiwa kukojoa kila mara kwa mara na kusaidia kusafisha njia ya mkojo.

Ni jambo linalosaidia kupunguza idadi ya wadudu wanaoweza kufika kwenye kibofu au kuzaliana.

Anatakiwa kujisafisha kutoka mbele kwenda nyuma ( klwa wanawake) na kuvaa nguo za ndani zisizobana sana na zilizotengenezwa kwa pamba na sio nguo zisizopitisha hewa.

***Mwandishi wa makala haya anapatikana kwa mawasiliano: jacpole@gmail.com***

AFYA

# Wenye ualbino wanaumizwa na mahitaji, kuchelewa matibabu

## • Ocean Road yawa 'mama kwa mwana'
## • Daktari: Ishara hizi, kimbilia hospitali

**Na Khadija Kalili**

WIKIENDI iliyopita nchini ilikuwa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wenye Ualbino Duniani.

Katika hilo, Dk. Kandali Samuel wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, anatoa wito kwa wenye ualbino kuwahi mapema hospitalini, wanapohisi mabadiliko ya kimwili, hali inayowasaidia kuwahi kukabiliana na madhara kama saratani ya ngozi.

"Nashauri kitaalamu kwamba, watu wenye ualbino ambao wengi wao hukumbwa na ugonjwa wa kansa ya ngozi, wawahi kuja hospitalini, pindi wanapoona kuna mabadiliko kwenye ngozi zao, hata wanapoona wakiandamwa na vipele mara kwa mara," anasema.

Katika mazungumzo maalum na Nipashe, Dk. Samuel anafafanua kwamba mtu unaweza kuhisi ni mabadiliko madogo mwilini, lakini uhalisi wake unaweza kujenga madhara makubwa kwa mhusika

"Mtu mwenye tatizo la ualbino ni bora akajijengea tabia ya kufanya uchunguzi mara kwa mara juu ya ugonjwa wa saratani, kwani anaweza kuona mabadiliko ni madogo, lakini pindi anapofanyiwa uchunguzi wa kina, hubainika ameathirika vibaya na saratani," anaeleza.

Daktari huyo anasema, hadi sasa Taasisi ya Ocean Road imeshasambaza huduma zake kuelimisha mikoani kuhusu saratani, ikiwa na mwongozo mahsusi unaohusu saratani na wenye ualbino wakipewa kipaumbele.

Hata hivyo, anakiri kuwapo changamoto ya wenye ualbino kusuasua kutibiwa hospitalini, hivyo anawataka kuripoti haraka ama Ocean Road au katika hospitali za mahali waliko, ambako wataaluma hao wa kansa sasa wameshawajengea uwezo katika ngazi ya mikoa.

Dk. Samuel anasema, taasisi ya Ocean Road ina kipaumbele cha kuwajengea uwezo wenye vituo vya afya, kuhusu ufahamu unaohusu saratani unaowaua, wengi wenye ualbino nchini.

Anasema tiba ya mionzi imekuwa na tafsiri tofauti miongoni mwa jamii, akitaja mionzi ni tiba maalum na salama, ikitoa dozi stahiki kwa mgonjwa.

Mtaalamu huyo anasisitiza kwamba, mtu anapoona amepatwa na mabadiliko ya ngozi awahi hospitalini kwani Kanza ikiwa katika hatua za awali inatibika.

Dk. Andrew anaeleza imani kwamba iwapo elimu ya kutosha itatolewa, watajitahidi kuweka kipaumbele hasa upande wa mikoani,



Katibu Mkuu wa Chama cha Watu Wenye Ualbino nchini, Mussa Kabimba (wa kwanza kulia juu na wa kwanza kushoto chini), akiwa katika matukio mbalimbali. **PICHA ZOTE:MAKTABA.**

> **"Wizara ya Afya wajumuishe unuuzi wa haya mafuta kinga ambayo kwetu siyo urembo, ni maisha yetu. Basi, wanapoagiza dawa kwa ajili ya Watanzania basi wakumbuke kutuletea na sisi mafuta kinga, ambayo ni sehemu ya maisha yetu na siyo urembo," anasema Kabimba.**

kuhakikisha huduma hii inawafika vizuri na kuokoa maisha ya watu wengi zaidi.

Kw mujibu wa Dk. Andrew, athari ya ngozi za ualbino hutokea mwilini katika pande zinazokutwa na mionzi ya jua ambayo ni kichwa, shingo na mikono.

### WALENGWA WALIKOFIKIA

Katibu wa klabu ya michezo ya Albinism Sports Club, Joseph Sinda, anaiomba serikani iwasaidie kwa Bohari Kuu ya Dawa, ichukue jukumu la kuwaagizia mafuta kinga kwa ajili ya watu wenye ualbino, ili waoate unafuu katika thamani ya bei.

" Wizara ya Afya wajumuishe unuuzi wa haya mafuta kinga ambayo kwetu siyo urembo, ni maisha yetu. Basi, wanapoagiza dawa kwa ajili ya Watanzania basi wakumbuke kutuletea na sisi mafuta kinga, ambayo ni sehemu ya maisha yetu na siyo urembo," anasema Kabimba.

Katibu Mkuu wa Chama cha Watu Wenye Ualbino nchini (TAS), Mussa Kabimba, anaiomba serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto dawa hizo zipatiwe hadhi sawa na zile za wagonjwa wa Ukimwi.

Kualimbiu ya mwaka huu katika maadhimisho hayo yanayohusu wenye ualbino yanasema "Haki sawa kwa wote boresha Afya, Elimu na Ajira kwa watu wenye Ualbino."

Pia, Kabimba anasema chama kwa kushirikiana na serikali, wamefanikiwa kukabidhi seti tisa za vifaa tiba vya saratani ya ngozi na kuzindua kliniki katika mikoa saba, anayoiyaja kuwa ni Dar es Salaam , Tanga, Lindi, Iringa, Singida, Mara na Unguja, kutanikisha kuwepo shauri wa kutosha juu afya ya ngozi zao.

"Uchunguzi wa mapema pamoja na tiba ya saratani, endapo ikipatikana mapema, pamoja na tiba ya saratani wakiwa kwenye mikoa yao, itasaidia kupunguza msongamano," anasema Kabimba.

Azma nyingine ya chama anaitaja ni kuhakikisha takwimu na taarifa zote zinazohusu saratani ya ngozi kwa watu wenye ualbino, zinaboreshwa.

Kabimba anataja mafanikio katika kuenea na taarifa zinazohusu seti ya vifaa tiba vya saratani ya ngozi, hadi kufikia tarehe 4 mwezi huu.

### TAKWIMU ZILIVYO

Kabimba anasema kuna jumla ya wenye ualbino 1501 waliowafikia na kati yao, 873 walikuwa wameungua, kuna 437 waliokuwa wameungua; 235 walipatiwa tiba ya dalili za saratani na wapo zaidi ya 60 waliopewa rufani zaidi katika hospitali kubwa.

Amataja mikoa iliyofikiwa na idadi ni: Tanga, wako 125 na kati yao waliokuwa na matatizo ni 95; Unguja waliofikiwa 112, wenye matatizo 84; Singida walifikiwa 258 na 230 walikuwa na matatizo; Iringa wenye matatizo ni 140.

Mikoa mingine, Lindi walifikiwa 74 na kati yao, wenye matatizo wako 50; Dodoma walifikiwa 70 na 52 walikuwa na matatizo; Mara ina 307 na wenye matatizo walikuwa 200.







# Wenye ulemavu waombewa NEC mazingira bora uchaguzi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Bethel Baptist Deaf of Tanzania (BBDCT), Frank Sarungi, ameiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuweka mazingira bora kwa watu wenye ulemavu kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba.

Sarungi alisema hayo jijini hapa wakati wa ufunguzi wa mradi wa uboreshaji wa mazingira shirikishi na wezeshi kwa watu wenye ulemavu katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Askofu Sarungi ambaye ni Mratibu wa Shirika la Kiroho Maalum kwa jamii ya watu wenye ulemavu wa usikivu, alisema kuwa makundi ya watu hao mara nyingi yanasahaulika katika kushirikishwa kwenye mchakato wa uchaguzi wa ngazi mbalimbali kutokana na kutowekewa mazingira shirikishi na wezeshi.

Alisema kutokana na umuhimu wa uchaguzi huo wanaiomba Tume hiyo kuandaa mazingira bora yatakayowawezesha kupata haki yao ya kimsingi ya kushiriki katika ushindani wa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Elimu Maalum, Joseph Degera, alisema kuwa pamoja na changamoto ya kukosa ushiriki pia kundi la watu wenye ulemavu wa kutosikia wanakosa taarifa mbalimbali kutokana na kukosa wataalamu wa lugha ya alama.

Mwalimu Degera alisema kundi hilo linachelewa kupatiwa taarifa na ratiba na kusababisha wengi kukosa ushiriki kwenye uchaguzi hata kama wana sifa inayowawezesha kugombea katika nafasi wanazozihitaji.

Naye, Ofisa Maendeleo ya Jamii mkoa wa Dodoma, Onorath Maiko, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha makundi ya watu wenye ulemavu yanapata haki zote za msingi.

Alisema haki hizo ni pamoja na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ikiwa ni pamoja na kuwapatia huduma za kijamii bila kubaguliwa kama vile haki ya kupata elimu, afya na ya kushiriki uchaguzi uchaguzi mkuu kwa wale ambao watakaojiona wana vigezo vya kushiriki katika nafasi ya urais, ubunge na udiwani.

# Jaji Mkuu aonya taasisi kuchelewesha haki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, amesema vitendo vya rushwa hushamiri zaidi katika taasisi zinazo chelewesha haki.

Amevitaka vyombo vya mahakama kupambana na vitendo hivyo ili kuepuka kuchelewesha haki.

Prof. Juma aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati alipokuwa akifungua kongamano la wadau kujadili rushwa katika mfumo wa utoaji haki nchini.

Alisema moja ya sababu za rushwa ni taasisi zinazohusika na utoaji wa haki kuchelewesha maamuzi, hivyo kufanya wananchi kuona kuwa wanatakiwa kutoa kitu ili maamuzi hayo yafanyike.

"Mapambano dhidi ya rushwa yasifanyike kwa sababu tu TAKUKURU yupo, bali yawe ni sehemu ya maisha yetu ya kila siku katika taasisi zetu ili kufanikiwa kuishinda rushwa," alisema.

Alisema, kama taasisi za utoaji haki nchini zinataka kufanikiwa katika mapambano dhidi ya rushwa ni lazima zishirikiane.

"Uzoefu unaonyesha kuwa rushwa haiwezi kumalizwa na mahakama pekee bali taasisi zote zinatakiwa kushirikiana ili kupunguza vitendo hivyo katika taasisi hizo au kuimaliza kabisa," alisema.

Aliwataka wadau hao kuacha kudharau mitazamo pamoja na hisia za wananchi katika suala la rushwa kwenye taasisi za utoaji haki nchini.

"Wananchi wamekuwa na mitazamo na hisia tofauti juu ya rushwa katika taasisi zetu, hivyo basi inatubidi kuona ni namna gani tunaweza kufanya ili kuijenga imani yao ambayo ndiyo silaha kubwa ya mapambano dhidi ya rushwa," alisema.

Vile vile, alisema muhimili wa mahakama nchini ndiyo unatakiwa kuwa mstari wa mbele kwenye mapambano dhidi ya rushwa na siyo kutegemea wadau walioko nje.

"Juhudi za kujisafisha lazima katika vita ya rushwa ni lazima vianzie ndani ya mahakama zenyewe ndiyo tuwe mstari wa mbele katika mapambano hayo na siyo kumtegemea mtu mwingine," alisema.

Naye, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Wilbert Chuma, alisema lengo la kongamano hilo ni kujadili hali ya rushwa katika vyombo vya utoaji haki nchini.

Alisema rushwa ni adui wa haki ambaye amekuwa akikemewa hadi katika vitabu vya dini hivyo taasisi zinazojihusisha na utoaji haki lazima zipambane kuitokomeza.



Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Dodoma, Onorath Michael, akizungumza na watu wenye ulemavu jijini humo kwenye semina ya uboreshaji wa mazingira shirikishi kwa ajili ya elimu ya uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka huu. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Wanaowania uongozi watakiwa kujipambanua

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MSTAHIKI Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, amewataka wanaowania nafasi ya udiwani kwenye kata za jijini Dodoma, wajipambanue na kujitathmini kwanza kabla ya kukimbilia madaraka hayo.

Prof. Mwamfupe aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na madiwani katika kikao cha kuvunja baraza hilo, jijini hapa.

Alisema watakaojitokeza kwenye nafasi hiyo ya udiwani ni muhimu wakajipambanua na kujitathmini kwanza, badala ya kukimbilia kwa kutaka madaraka hayo bila kufikiri jinsi watakavyotumikia wananchi.

Alisema kuwa lengo la serikali iliyopo madarakani ni kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo, hivyo watakaojitokeza waweke maslahi ya wananchi kwanza badala ya kufikiria nafasi hiyo ya udiwani.

"Watu wanapenda kuona maendeleo na siyo udiwani ulionao kwa kuwa hicho ni cheo tu ukizingatia wananchi wanapenda kuona yale yaliyoahidiwa yametekelezwa kwa manufaa ya nchi, hivyo tunapohitimisha baraza hili ni imani yangu mtakwenda kuomba kura ili muwatumikie wananchi wenyewe na raslimali zilizopo," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, akisoma

**Watu wanapenda kuona maendeleo na siyo udiwani ulionao kwa kuwa hicho ni cheo tu ukizingatia wananchi wanapenda kuona yale yaliyoahidiwa yametekelezwa kwa manufaa ya nchi, hivyo tunapohitimisha baraza hili ni imani yangu mtakwenda kuomba kura ili muwatumikie wananchi wenyewe na raslimali zilizop**

taarifa ya mafanikio yaliyopatikana katika jiji hilo mbele ya madiwani, alisema kuwa wamefanikisha kuwapo kwa maendeleo makubwa yaliyotokana na miundombinu mbalimbali ya kitaifa na ya kisasa kama vile ya barabara, afya, elimu, upimaji wa ardhi na utatuaji wa migogoro ya ardhi na majengo ya kiofisi na ujenzi wa nyumba zilizojengwa kwa mpangilio.

Alisema kuwapo kwa mafanikio hayo uchumi umeongezeka kwa kasi kubwa kuliko huko nyuma kutokana na ukusanyaji wa mapato ambayo hayawezi kulinganisha na halmashauri zozote nchini.

Alisema kuwa kutokana na maendeleo ya Dodoma ni imani yake kuwa madiwani hao wanaomaliza muda wao wataomba kurudi kwenye nafasi zao kwa kifua mbele kutokana na ushirika wao waliouonyesha kati yao na wananchi pamoja na halmashauri ya jiji na kufanikisha kuwapo kwa miradi mikubwa

## HABARI MBEYA



Baadhi ya wananchi wa eneo la Uyole jijini Mbeya, wakiangalia namna moto uliozuka na kuunguza vitu vyote vilivyokuwamo katika nyumba hiyo . **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

# Wakulima wa mboga, matunda wapata fursa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JUMLA ya wakulima 7,500 kutoka Halmashauri za mikoa mitatu ya Mbeya, Songwe na Katavi watafikiwa na programu ya mboga na matunda ili kuongeza tija ya uzalishaji, kuongeza upatikanaji wa chakula na usalama wake.

Aidha, programu hiyo lengo lake ni kuboresha hali ya lishe ukanda wa Nyanda za Juu Kusini.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa Programu hiyo wa Shirika la Helvetas, linalojihusisha na kilimo, Nyanda za Juu Kusini, Daniel Kalimbiya, wakati wa warsha iliyowahusisha maofisa kilimo.

Kalimbiya alisema programu hiyo ni ya miaka minne ambapo imeanza mwaka huu na inavinufaisha vikundi vya wakulima 500 pamoja na vyama vya ushirika vinavyojihusisha na kilimo cha mboga na matunda.

"Mradi huu wa miaka minne ambao ulianza Mei 2020 hadi kukamilika kwake utawafikia wakulima wa mboga na matunda wapatao 7,500 kutoka kaya 1,500 ili kuongeza tija na thamani kwenye mazao hayo sambamba na ujenzi wa viwanda ili kusaidia usindikaji wa kwa sababu mazao mengi yanapotea licha ya kuyahifadhi. Pia kuwatafutia masoko na kutoa elimu ya uzalishaji bora ili kukidhi viwango vinavyohitajika, kitaifa na kimataifa," alisema Kalimbiya. Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya Idara ya Uchumi na Uwekezaji, Said Madito, alilipongeza shirika hilo kwa kuunga mkono serikali kwa kuanzisha programu hiyo na kuyalenga makundi na wanawake na vijana kwa kuwa ndio wazalishaji wakubwa.

Alisema shirika linapaswa kuongeza thamani ya mnyororo wote mazao kwa kuhakikisha uzalishaji kilimo hicho unafanikiwa ili kuleta matokeo chanya.

Alilishauri shirika kwamba baada ya programu hiyo kumalizika, wafanye tathmini ambayo itaonyesha kama malengo yao wameyafikia pamoja na ufuatiliaji wa mradi huo ili kutambua matokeo ya kile walichokifanya kwa kipindi cha miaka minne.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema Shirika la Helvetas kwa kushirikiana na kituo hicho, watahakikisha wanawanufaisha wakulima kuwapatia elimu, kuwatafutia masoko na kuwajengea viwanda vya usindikaji.

Alisema katika programu hiyo itaweza kuwanufaisha wananchi milioni moja ingawa sio moja kwa moja kupitia usambazaji wa pembejeo za kilimo, wauzaji wa walaji wa mazao au bidhaa zitakazozalishwa.

"Kituo cha TARI- Uyole katika programu hiyo kimejikita katika kushauri aina ya mbegu zinazofaa kutumika, lishe kwa kutoa ushauri wa aina gani ya chakula kinachofaa kitumiwa pamoja na matumizi bora ya pembejeo za kilimo," alisema Dk. Bucheyeki.

Ofisa Kilimo Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Merius Nzalawahe, anayeshughulikia mazao ya bustani, alisema mazao hayo, yana faida kubwa kwa sababu yanatumia eneo dogo, lakini mavuno yanakuwa mengi ukilinganisha na mengine, hivyo aliwahimiza wakulima kujikita katika eneo hilo.

Alisema serikali imeendelea na jitihada zake za kuhamasisha kilimo cha mboga na matunda kwa kuwahimiza waendelee kuongeza maeneo kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo hicho.

# Ataka orodha ya migogoro ya ardhi

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

KAMISHNA Msaidizi wa Ardhi mkoani Mbeya, Jeremiah Minja, ameziagiza halmashauri zote za mkoa wa Mbeya kuhakikisha zinaandaa orodha ya migogoro yote ya ardhi ambayo inaweza kutatuliwa na ofisi yake kwa wakati.

Amesema lengo ni kuepusha migogoro isiyo ya lazima kuendelea mkoani humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema kumekuwapo na migogoro katika ngazi za halmashauri ambayo inaweza kutatuliwa kwa wakati katika ofisi hiyo ya ardhi mkoani Mbeya badala ya kuwaacha wananchi wakihangaika.

Alisema uamuzi wa serikali kuanzisha ofisi za ardhi ngazi ya mkoa unakusudia kuharakisha utatuzi wa migogoro mbalimbali ya ardhi katika ngazi za halmashauri na kuwa ofisi hiyo imejipanga kuhakikisha migogoro hiyo inapungua haraka iwezekanavyo na kuondoa adha ya walalamikaji kuhusiana na mambo ya ardhi.

Alisema tangu kuanzishwa kwa ofisi hiyo ngazi ya mkoa, imeshashughulikia migogoro mbalimbali ya ardhi iliyo ndani ya uwezo kwa kuwa suala hilo lipo kwenye mpango, inaendelea kukusanya maduhuli ya serikali ipasavyo ambayo yanatokana na pango la ardhi na kodi ya majengo pamoja na kuhakikisha miji yote ndani ya mkoa huo inapangwa, inapimwa na kutoa umiliki halali.

"Unajua tumechoshwa na ujenzi holela wa makazi ya wananchi ndani ya mkoa wa Mbeya na kuwa kuanzia sasa tupo katika mkakati wa kupima viwanja katika maeneo ya miji ili kuhakikisha wananchi wanamiliki viwanja vilivyopimwa," alisema.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilikopa Sh. milioni 639 kutoka mfuko wa kupima viwanja Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika eneo la Mbeya Peak (Iziwa) na kuwa mpango huo ulifanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Minja alisema wana mpango wa kuelekeza shughuli za upimaji wa viwanja katika eneo la Iduda jijini Mbeya pamoja na kuliweka jiji hilo katika mpangilio wa makazi.

Alisema pia alisema wamefanikiwa kutoa hati za kimila 10,837 kwa wananchi kwa lengo la kuwawezesha kuwa na umiliki halali wa ardhi katika maeneo yao.

Minja alisema hati za kimila zina umuhimu sana katika maisha ya kila siku ya wananchi kwa kuwa inamwezesha mwananchi kuwa na ummiliki halali na kuweza kuaminika kirahisi na taasisi za kifedha kwa lengo la kupata mikopo.

Alisema kwa mjibu wa takwimu za mwaka za kuanzia mwezi Julai, 2019 hadi Machi 2020, ofisi ya ardhi mkoa wa Mbeya imefanikiwa kugawa hati za kimila 10,837 kwa wananchi katika maeneo tofauti ya mkoa.

Akitolea mfano, Minja alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Vijijini jumla ya hati za kimila 9,879 zimegawiwa kwa wananchi, hati 732 zimegawiwa katika Halmashauri ya Mbarali na hati 129 zimegawiwa katika Halmashauri ya Rungwe.

Pia alisema katika Halmashauri ya Busokero jumla ya hati 57 zimegawiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kuna hati 38 zilizogawiwa na katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kuna hati mbili tu zilizogawiwa.

# Moto wakosesha makazi familia nane

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

FAMILIA nane katika mtaa wa Mwanyanje, Kata ya Uyole jijini Mbeya hazina mahali pa kuishi baada ya nyumba zao kuteketea kwa moto.

Moto huo ulizuka juzi mchana wakati baadhi ya wanafamilia hao wakiwa ndani ya nyumba, hata hivyo walinusurika baada ya kutimua mbio.

Akizungumza na gazeti hili, mmoja wa shuhuda wa tukio hilo, Kenedy Edison, alisema kuwa waliona moshi mwingi ukifukuta ndani ya nyumba hiyo kabla ya moto kulipuka.

"Tulikuwa tunafanya kazi zetu jirani na nyumba hii, tukaona moshi mwingi ukitokea madirishani na ghafla moto mkubwa ukalipuka kiasi kwamba hatukuweza hata kuingia ndani kuokoa vitu vilivyokuwamo," alisema Edson.

Wapangaji wa nyumba hiyo ambayo pia ilikuwa na maduka matatu ndani yake, walisema mbali na kukosa mahali pa kuishi pia mali zao zote zimeteketezwa na moto huo.

Edmund Dinya, mpangaji ndani ya nyumba hiyo, alisema kuwa wakati nyumba hiyo inawaka moto, hakuwepo na hivyo hakuweza kuokoa vitu vyake vyote.

"Kwa kweli mbali na kwamba hatuna mahali pa kuishi, lakini tumepata hasara kubwa kwa sababu hatukuweza kuokoa mali zetu zilizokuwa ndani ya nyumba ambazo zote zimeteketea kwa moto," alisema Dinya.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mwanyanje, Joseph Ndambo, alisema baada ya kupata taarifa ya tukio hilo, alitoa taarifa kwa kuwapigia simu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambao waliwahi na kuuzima.

Alisema askari wa Jeshi la Zimamoto walijitahidi kuwahi, lakini kutokana na umbali ilipo ofisi yao, walipofika walikuta nyumba yote imeshashika moto hivyo walichokifanya ni kuuzima na hawakuweza kuokoa mali zilizokuwamo.

"Ofisi za Zimamoto zipo mjini, umbali wa takriban kilometa 12 kutoka hapa Uyole, nilipowapigia tu simu walikimbia kuja, lakini mpaka wanafika hapa walikuta moto umeishaizingira nyumba nzima hivyo wakaanza kuuzima na hawakuokoa kitu chochote," alisema Ndambo.

Mmiliki wa nyumba hiyo Bosco Ngogo, alisema hakuna mtu yeyote aliyedhurika kwa moto huo ingawa mali zake na wapangaji wake zimeteketea zote kwa moto huo.



# Wazazi waonywa kuozesha watoto katika umri mdogo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Kijiji cha Sos, Asha Salum, amewataka wazazi kuacha kuwafungisha ndoa watoto wenye umri mdogo ambao bado wanahitaji kupata elimu.

Aliyasema hayo katika kijiji hicho Mombasa Mjini Unguja katika kilele cha Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo huadhimishwa ifikapo Juni 16 kila mwaka.

Alisema kuwa watoto wanahitaji kupatiwa haki zao ikiwamo haki ya elimu, hivyo kuwaozesha mapema ni kumvunjia haki yake.

Mkurugenzi huyo alimpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein, kwa kuipa kipaumbele sekta ya elimu na kuendeleza misingi ya Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume ya kutoa elimu bure.

Aliwataka watoto kuitumia fursa hiyo na kusoma kwa bidii ili kuweza kufanikiwa katika maisha yao ya baadaye.

"Kabla ya mwaka 1964 wazee wetu walikosa fursa ya kupata elimu na elimu ilikuwa ikitolewa kwa ubaguzi, lakini hivi sasa elimu bure kwa watu wote watoto someni ili nchi iweze kupata wataalamu," alisema.

Aidha, mkurugenzi huyo alimpongeza Rais msataafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ali Hassan Mwinyi, kwa kuruhusu kuanzishwa kwa kituo cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu SOS, ambapo hivi sasa ni miaka 73 tangu kuanzishwa kwa kituo hicho Zanzibar.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu kutoka katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Suleiman Yahya, alisema kuwa elimu ni silaha pekee ambayo inaweza kuleta mabadiliko.

Alisema katika kuimarisha mifumo ya elimu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imeanza kupitia mtaala wa elimu ambao utazingatia masuala ya udhalilishaji.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu, Suleiman Yahya, akimkabidhi zawadi mwanafunzi wa Shule ya Kinuni, Mwanaisha Vuai, katika kilele cha Siku ya Mtoto wa Afrika, ambaye amefanya vizuri katika uandishi wa insha. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri aitaka tume kutoa elimu ya sheria kwa jamii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba na Sheria amewataka wanasheria kutoa elimu ya sheria kwa jamii ili iweze kuepuka makosa ya uvunjaji wa sheria.

Akizindua jarida lililoandaliwa na Tume ya Kurekebisha Sheria, waziri huyo alisema jarida hilo litasaidia wananchi kupata elimu ya sheria na kupungua kwa makosa ya uvunjaji wa sheria.

Waziri huyo alitaka Tume ya Kurekebisha Sheria kuzifanyia marekebisho sheria zilizopitwa na wakati ili kwenda na wakati uliopo.

Pia, aliitaka tume hiyo kuwashirikisha wananchi wakati wanapotunga sheria ili kuweza kutoa maoni yao na kufanyiwa kazi.

Alieleza kuwa si vyema kwa watendaji wa tume hiyo kukaa mezani na kutoa mapendekezo yao bila ya kuwashirikisha wananchi ambao ndio walengwa wa sheria.

"Mwende mjini na vijijini kuchukua maoni ya wananchi ili kuchukua maoni na kuhakikisha kila kundi linapewa nafasi kabla ya marekebisho kufanywa," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Jaji Bakari Mshibe, alisema kuwa tume hiyo itakua inatoa jarida la elimu ya sheria kila mwaka na kuligawa kwa wananchi ili kuwa na uelewa wa masuala hayo.

Kwa upande wake, Katibu wa Tume hiyo, Kubingwa Mashaka Simba, alisema tume imelenga kukuza uelewa kwa jamii kuhusu uwelewa wa utawala wa sheria.

# JPM amwagiwa sifa uongozi uliotukuka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Magufuli, kwa utendaji wake mzuri, ukiongozwa na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2021, hatua ambayo inatoa nafasi na fursa kubwa kwa CCM kushinda tena katika uchaguzi mkuu ujao.

Wakizungumza katika Baraza la Wawakilishi, Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe, Omar Chande, alisema katika kipindi cha utendaji wa kazi cha miaka mitano, Magufuli amefanya mambo makubwa, ikiwamo kuimarisha uchumi na kulinda rasilimali za taifa kumilikiwa na wananchi wazalendo.

Alisema hatua hizo zimekuja baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano kupitisha sheria ambazo zinamilikisha utajiri wa rasilimali za madini mikononi mwa wananchi.

"Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi zangu za dhati kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kwa kufanya mambo makubwa katika kipindi cha miaka mitano tu uongozi wake...ameifanya kazi ya ushindi wa CCM katika uchaguzi ujao kuwa nyepesi sana," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Chonga, Shaibu Said, alisema Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano imekuwa na utulivu mkubwa wa kisiasa kutokana na juhudi zilizochukuliwa na Rais Magufuli.

Alisema hatua hiyo imetoa nafasi nzuri kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya shughuli zake za kiuchumi ikiwamo kuimarika kwa utalii na mapato yake.

"Kwa niaba ya wananchi wa kisiwa cha Pemba tunampongeza Rais John Magufuli kwa kuiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kushirikiana na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein na kuivusha Jamhuri katika maendeleo, amani na utulivu mkubwa," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake, Suleiman Sarhani, alisema wakati taifa la Tanzania likielekea katika uchaguzi mkuu, wananchi wakipigie kura Chama Cha Mapinduzi kwani mambo kiliyoyafanya katika kipindi cha miaka mitano ni makubwa.

"Wananchi tusifanye majaribio katika siasa na uongozi... mambo yaliyofanywa na Rais Magufuli pamoja na Dk. Shein katika kipindi cha miaka mitano ni makubwa," alisema.

HABARI KITAIFA

# TRAWU yalalamikia muundo wa utumishi

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

CHAMA cha Wafanyakazi wa Reli Tanzania (TRAWU) kimeeleza kutoridhishwa na muundo mpya wa utumishi kufuatia uundaji wake kutoshirikisha chama cha wafanyakazi pamoja na kubaini upungufu kadhaa.

Miongoni mwa upungufu huo ni uwiano wa wafanyakazi, huku ikiacha zaidi ya asilimia 80 ya wafanyakazi katika hali ya sintofahamu juu ya hatma yao baada ya kustaafu.

Akitoa maadhimio ya kikao maalumu cha kamati kuu ya chama hicho Kaimu Mwenyekiti wa TRAWU taifa, Xavier Marko, alisema kuwa walifikia maazimio hayo kufuatia muundo huo mpya wa utumishi kubainika na kuwa na upungufu katika baadhi ya vipengele.

Alisema kuwa baadhi ya vifungu ambavyo vimeleta ukakasi katika muundo huo ni kutotambua thamani ya wafanyakazi ambao walikuwa wakikaimu nafasi mbalimbali tangu mwaka 1997.

"Hii scheme of service (muundo wa utumishi) imewaacha wafanyakazi zaidi ya asilimia 80 katika hali ya sintofahamu, kuna wastaafu na hata wale ambao walikaimu nafasi tangu 1997 hawana uhakika juu ya hatima yao," alisema na kuongeza:

"Imewabagua sana wafanyakazi kwa kuwa imeanza kutumika bila kushirikisha chama na wafanyakazi."

Aliongeza kuwa chama hicho kimeazimia kuandika barua Shirika la Reli (TRC) na serikali kufuata utaratibu wa kuitisha kikao maalum cha majadiliano ili kujadili na kufanya marekebisho ya muundo huo.

Kwa upande wake, Kaimu Katibu Mkuu wa TRAWU, Shehe Shuhuli, alisema kuwa changamoto nyingine zinazowakabili wafanyakazi wa reli ni madeni makubwa ambayo wanadai TRC kufuatia waajiri wao kutowasilisha michango ya wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

Alifafanua kuwa tangu mwaka 2015 makato yao hayajapelekwa katika mifuko ya PSSF na WCF, jambo lililopelekea baadhi ya wafanyakazi kutolipwa mafao yao kwa muda marefu.

"Wastaafu wengi hawajalipwa mafao yao kwa muda sasa kutokana na michango yao katika mifuko ya hifadhi ya jamii na Saccos kutowasilishwa sehemu husika, tunamuomba Rais Magufuli kuingilia kati suala hili ili wastaafu wapate haki zao," alisema Shuhuli.

# Bosi wa TAKUKURU atoa onyo kali uchaguzi mkuu

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), imetoa rai sita kwa wagombea na Watanzania kujiepusha na vitendo vya rushwa kwenye Uchaguzi Mkuu 2020, huku ikisema yeyote atayakebainika ataonja joto la jiwe la kisheria.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbungo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu rai ya TAKUKURU kuelekea uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Alisema uchaguzi unapogubikwa au kuhisiwa kujitokeza vitendo vya rushwa unakosa uhalali wa kisheria na kisiasa na hivyo kusababisha uvunjifu wa amani.

"Napenda kusisitiza kuwa rushwa yoyote iwe ni ndogo ya Sh.10,000 au Sh.50,000 itakayotolewa na mtia nia au mgombea yeyote inaweza kukugharimu mwananchi kwa kukosa maendeleo na kutokuwa na utatuzi wa changamoto zinazozunguka maisha ya kila siku ya wewe mpigakura kwa kipindi cha miaka mitano," alisema.

Aliwataka Watanzania kutambua kuwa mgombea au Mtiania ya kutaka kuchaguliwa akishatoa rushwa, yeye atajikita zaidi katika kurejesha fedha alizotumia kuhonga na hata jali maendeleo yao.

"Kutokana na hilo, Takukuru inatoa rai kwa kila Mtanzania kwanza kuzingatia yale yote ambayo tumekuwa tukiwaelimisha kuhusu madhara ya rushwa, pili kuzingatia yale yote tuliyokubaliana kwenye warsha na kuweka mikakati," alisema.

Pia, alisema rai ya tatu ni kuzingatia sheria, kanuni, taratibu za uchaguzi na kutojihusisha na rushwa wakati wote wa mchakato wa uchaguzi wa 2020.

"Rai ya tano ni kutoa ushirikiano kwa Taasisi hiyo na ninasisitiza tena kila anayehusika kwenye mchakato wa uchaguzi ajiepushe na vitendo vya rushwa," alisema.

Alisema kila wakati wa uchaguzi kunakuwa na malalamiko kwamba kuna wakati wanaojihusisha na vitendo vya rushwa.

"Malalamiko haya yanatolewa na Watanzania wenzetu wakadai wapo baadhi ya Watanzania wenzetu wanajihusisha na vitendo vya rushwa, ninapenda pia kuwakumbusha kuwa Ibara ya 9(h) ya Katiba inatutaka tuelekeze nguvu na juhudi zetu zote kwa lengo la kuhakikisha hakuna dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu au upendeleo zinaondolewa nchini," alisema.

Alisisitiza kuwa wananchi wanaotaka kugombea uongozi wajitathimini kama wana uwezo na sifa za kiongozi nchini.

"Waandishi pia mjiepushe kutumika kiasiasa katika kutoa taarifa za kampeni au kutoa taarifa zenye mwelekeo wa kirushwa na uchochezi," alisema.

Aliwataka wasimamizi wa uchaguzi kutimiza wajibu wao ipasavyo kama vile kusimamia na kufuata sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi.




Wachuuzi wa miwa wakisaka wateja kwa kutumia baiskeli ya matairi matatu(GUTA) katikati eneo la Urafiki, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# HakiElimu yataka mbinu mbadala uboreshaji mfumo wa elimu

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI isiyo ya serikali ya HakiElimu imesema kuna haja ya kujifunza mbinu mbadala ambazo zitasaidia kuboresha zaidi mfumo wa elimu nchini hususani kunapotokea majanga kama ya ugonjwa wa Corona.

Akifungua mjadala wa kujadili namna ya kusonga mbele na kuwa na mfumo bora zaidi wa utoaji elimu nchini hususani kunapotokea majanga, Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, John Kalaghe, alisema ni muhimu kwa serikali na wadau wengine kuendeleza mijadala zaidi juu ya upatikanaji wa elimu katika vipindi vya majanga hayo..

Kalaghe alisema ni vizuri kuja na mipango itakayosaidia kufidia ombwe la ujifunzaji lililoletwa na kufungwa kwa taasisi za elimu hususani katika kipindi cha tishio la ugonjwa wa Corona.

"Tunapendekeza pia kuzitumia changamoto zilizotokana na janga la corona kuwa fursa katika kujifunza namna bora ya kuimarisha mfumo wa elimu ili uwe nyumbufu na unaokidhi matakwa ya utoaji wa elimu na unaoendana na mahitaji ya karne ya 21,"alisema Kalaghe.

"Tunapendekeza pia kuwekeza kwa nguvu katika matumizi ya teknolojia katika utoaji elimu kwa watoto wetu. Ni lazima mabadiliko yafanyike juu ya ni namna gani shule zinaweza kutumia teknolojia zaidi kufikia maarifa yanaoyokusudiwa."

Kalaghe alisema vipindi vya majanga makubwa kama hayo, vinapaswa kutumika kama fursa ya kuleta mabadiliko ya namna ya kuwekeza katika uendeshaji wa shule na taasisi za elimu nchini hususani kwa kuimarisha na kutatua upungufu wa miundombinu na mfumo wa Tehama kwa ajili ya kurahisisha ujifunzaji.

"Changamoto iliyoletwa na COVID_19 inapaswa pia iwe ni fursa kwetu ya kutafakari namna ya kuimarisha mifumo yetu ya ulinzi wa mtoto awapo shuleni au nyumbani. Lakini pia changamoto na uzoefu tuliopitia kipindi hiki, vinapaswa kuwa fursa ya kufanya marekebisho ya sheria za kodi, tozo na uwezeshaji wa wananchi katika matumizi ya teknolojia," alisema Kalaghe.

"Hii inaweza kuanza na kuhusisha elimu ya teknolojia kuanzia elimu ya awali na kuendesha vipindi vya kuwajengea uwezo wazazi, walezi, walimu na kuwahamasisha juu ya matumizi ya teknolojia."

Kalaghe alisema zipo njia mbadala ambazo zilipendekezwa na wanafunzi zitumike katika kujifunzia wakati wa kipindi chote cha ugonjwa wa corona na kwamba ni vema pia njia hizo zikatumika kuwafikia watoto na makundi ya watoto walio nje ya mfumo rasmi wa shule na waishio katika mazingira magumu.



# ARTETA

## ATAKA KUMBAKISHA LUIZ ARSENAL

**LONDON, England**

KOCHA mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta amesema "angependa" kumbakisha mlinzi, David Luiz klabuni hapo.

Luiz mwenye umri wa miaka 33, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil aliwasili pale Arsenal mwaka jana na amecheza mechi 32 msimu huu kabla ya jana Jumatano dhidi ya Manchester City.

Arteta anataka kumbakisha mlinzi huyo wa zamani wa Chelsea Luiz, akisema alikuwa muhimu kwa timu yake.

"Kwa uhakika nina furaha na David, nataka kumbakisha yeye hapa na sisi. Amekuwa nguzo muhimu tangu alipojiunga," amesema Arteta.

"Napenda kile anachokifanya dimbani, napenda ushawishi wake kwa wachezaji na klabu.

"Nataka kumbakisha."



## SETIEN AMTAKA FATI KUIMARIKA ZAIDI

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Quique Setien, anataka kuona kiwango cha juu zaidi kutoka kwa fowadi wake kinda, Ansu Fati.

Fati alifunga bao la kwanza wakati Barcelona wakiibuka na ushindi wa 2-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, dhidi ya Leganes, Jumanne, na kufikisha mabao sita aliyofunga msimu huu.

Setien ana matumaini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 ataimarika zaidi, ambaye alitolewa nje kipindi cha pili wakati timu yake ikiibuka na ushindi huo.

"Tunataka kucheza na Ansu Fati amekuwa akifanya mazoezi vizuri sana. Nina furaha na uwezo wake," alisema kocha huyo akiwaambia waandishi wa habari.

"Alifanya kazi nzuri. Bila shaka yoyote amekuwa akifunga mabao na kufanya maisha kuwa magumu kwa walinzi. Ni kweli kwamba ana kazi kubwa ya kufanya.

"Anahitajika kuendelea kuwa na kiwango cha juu ambacho sasa bado hajafika, pengine ni kwa sababu ya kusumbuliwa na majeruha ya mara kwa mara.

"Lakini amekuwa akicheza vizuri sana na hatukutaka kutaharisha afya yake na hivyo naamini atazidi kuimarika."

Lionel Messi alifunga bao la pili kwa Barcelona kwa mkwaju wa penalti wakati wakiendelea kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

## Silva kuagwa kiaina yake Man City

**MANCHESTER, England**

DAVID Silva atamaliza msimu na Manchester City na "ataagwa vizuri sana", kocha Pep Guardiola amesema.


Silva mkataba wake unamalizika Juni hii na alithibitisha kwamba, huu ndio msimu wake wa mwisho kucheza hapo kwenye uwanja wa Etihad.

Na Guardiola ana matumaini kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye amekuwa kwenye Ligi Kuu ya England tangu mwaka 2010, ataagwa vizuri zaidi.

"Ndio, David atabakia hapa hadi mwishoni mwa msimu," alisema akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa jana Jumatano kati ya City na Arsenal.

"Atamaliza mechi zake za mwisho hapa bila mashabiki, lakini matumaini yangu yeye na klabu wameandaa kitu kizuri kwa ajili ya kuagwa kwake.

"Klabu kubwa zinakuwa za kuvutia zaidi wakati zinapoachana na wachezaji ambao wamekaa nao kwa zaidi ya muongo mmoja...kama Vincent Kompany, Joe Hart, Yaya Toure."



# LEIPZIG YAKOMAA NA WERNER



**DORTMUND, Ujerumani**

TIMO Werner bado yupo kwenye mipango ya RB Leipzig kwa ajili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya licha ya ripoti kuwa ameiarifu klabu hiyo anataka kwenda Chelsea kabla ya mashindano hayo kuanza tena.

Leipzig iliwaondoa Tottenham Hotspur na kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya msimu huu wa 2019-20 kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Ulaya itaendelea Agosti baada ya ligi zote kumalizika.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka gazeti la Bild la Jumatatu, Werner ameiambia Leipzig anataka kujiunga na Chelsea, ambao sasa hawatalipa kiasi cha euro milioni 53 zilizopo kwenye mkataba wake, baada ya kumalizika kwa msimu wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, mwezi huu.

Hata hivyo, bosi wa Leipzig, Julian Nagelsmann amewaambia waandishi wa habari bado anafikiria straika huyo wa Ujerumani atakuwapo kwa ajili ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kwa sasa tupo naye ni mipango yangu ni kuwa atakuwepo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Yeye ni mchezaji wetu na hajasaini mahali pengine," amesema Nagelsmann.

"Umuhimu wake kwa RB Leipzig ni wa aina yake. Ana uwezo mkubwa wa kufunga mabao mazuri, kitu ambacho mara zote ni kizuri kwa mshambuliaji."

## SIJAZUNGUMZA NA BAYERN KUHUSU HAKIMI – WAKALA

**MUNICH, Ujerumani**

BAYERN Munich hawajafanya mawasiliano yoyote na Real Madrid juu ya mpango wa kumsajili Achraf Hakimi, kwa mujibu wa wakala wa mchezaji huyo anayecheza kwa mkopo Borussia Dortmund.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Hispania zilizoandikwa na gazeti la AS, Bayern wapo tayari kutumia kiasi kikubwa cha fedha kama ada na mshahara kwa ajili ya kumsajili Hakimi kutoka kwa miamba hao wa LaLiga, Madrid.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco mkataba wake wa mkopo wa miaka miwili pale Dortmund unatarajia kumalizika mwishoni mwa msimu huu, ingawa klabu hiyo imeonyesha nia ya kutaka abaki.

Wakala wa Hakimi, Alejandro Camano amesisitiza Bayern hawajatoa ofa yoyote kwa mlinzi hiyo, ambaye bado amebakiwa na mwaka mmoja katika mkataba wake na Madrid.

"Kuna klabu kubwa zinamtaka, lakini sijui chochote kuhusu uvumi wa Bayern unakotoka," amesema Camano akiiambia Goal and SPOX.

"Hakuna mtu yoyote kutoka Bayern au Real Madrid ambaye amezungumza na mimi kuhusu uwezekano wa uhamisho wa Achraf kwenda Bayern."

Hakimi amecheza mechi 16 kwa Madrid msimu wa 2017-18 na Camano amebainisha kwamba, mlinzi huyo ana mahusiano mazuri sana na kocha wa Madrid, Zinedine Zidane.





## Man United yatajiwa bei ya Grealish

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Aston Villa inataka angalau pauni milioni 80 kwa ajili ya kumwachia Jack Grealish anayehusishwa na mpango wa kutakiwa kule Manchester United, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Man United wanajua kwamba watahitaji kulipa kiasi kikubwa cha fedha kwa Aston Villa kwa ajili ya kumsajili nahodha wake huyo, Grealish.

Kwa muda mrefu Grealish amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa pale katika dimba la Old Trafford baada ya kuwa ma msimu wa kuvutia kule Villa.

Hata hivyo, Man United wanaweza kumpata mchezaji huyo wa bei rahisi kama Aston Villa itashuka daraja msimu huu.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka ndani ya Villa pia wao wanamatumaini ya kumbakisha kiungo huyo na kikubwa kwa sasa wanapigana kutoshuka daraja.

Grealish mwenye umri wa miaka 24, amefunga mabao sana na kutoa pasi za mwisho sita katika mechi 26 za Ligi Kuu msimu huu.

Mwisho.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LEWANDOWSKI: SASA NATAKA TAJI LA UEFA

●●●Ni baada ya kuiwezesha Bayern kutwaa ubingwa wa Bundelisga msimu huu ...

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski anataka kuona mengi zaidi kutoka Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, baada ya kubeba kombe la Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, usiku wa kuamkia jana.

Bao la Lewandowski la kipindi cha kwanza liliinyanyua Bayern kupata ushindi wa 1-0 dhidi ya Werder Bremen Jumanne, na kubeba taji lake la nane licha ya kadi nyekundu ya Alphonso Davies dakika za majeruhi.

Vijana hao wa Hansi Flick wapo kwenye nafasi nzuri ya kutinga robo fainali Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Chelsea kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya mtoano wa timu 16, huku mashindano hayo yakitarajiwa kumalizika Agosti.

Lewandowski, ambaye amefunga mabao 46 msimu huu, ana matumaini Bayern inaweza kufikia mafanikio mengine makubwa Ulaya kwa kubeba kombe la mashindano hayo.

"Sisi ni mabingwa wa Ujerumani. Bila shaka inahuzunisha kidogo kusherehekea bila mashabiki uwanjani. Kwa hali fulani msisimko wa aina yake umekosekana," amesema straika huyo akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

"Bado tumeridhishwa sana. Haukuwa msimu rahisi, tulipambana kwa ajili ya taji kwa muda mrefu. Natumaini kwamba tunaweza kusherehekea pamoja na mashabiki wetu uwanjani hivi karibuni.

"Werder walicheza kwa staili ya kuzuia sana, lakini tulicheza vizuri kipindi cha kwanza.

"Tulionyesha kwamba sisi ni timu bora Ujerumani na tunataka kucheza kwa ubora zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nina hakika sasa nguvu na akili ya kila mchezaji itaelekezwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ili tuweze kujihakikisha nafasi ya kulibeba taji hilo.

"Tayari tupo kwenye nafasi nzuri ya kutinga robo fainali, kwa sababu kwenye mchezo wa kwanza tayari tunaongoza kwa mabao 3-0 dhidi ya Chelsea. Najua kwamba inaweza kuwa sio kazi rahisi, lakini nina imani tuna nafasi nzuri."

Bayern bado imebakiwa na mechi mbili kumaliza Bundesliga msimu huu, ambapo itacheza na Freiburg Jumamosi kabla ya kuwavaa Wolfsburg wiki moja baadaye.

## KWA UFUPI

**MAN UNITED YAMWANIA WILLIAN**

MANCHESTER United imefanya mawasiliano na wawakilishi wa Willian ili kukubaliana kuhusu uhamisho huru kwa fowadi huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 31, ambaye mkataba wake pale Chelsea unamalizika kipindi hiki cha majira ya joto. ***(France Football)***

**ASTON VILLA YATAKA MIL. 80 KWA GREALISH**

KLABU ya Aston Villa inataka angalau pauni milioni 80 kwa ajili ya kumwachia kiungo wake Muingereza, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 24, wakati dirisha la usajili litakapofunguliwa na hawajakata tamaa ya kumbakisha nahodha wao huyo kama wasiposhuka daraja. ***(Mail)***

**LAMPARD AMWINDA BENRAHMA**

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard anamwania winga wa Brentford, Said Benrahma, lakini Leicester City pia wanawania kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 raia wa Algeria. ***(Express)***

**ANCELOTTI ATAKA KIUNGO NAPOLI**

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti amefungua mazungumzo na klabu yake ya zamani ya Napoli juu ya usajili wa kiungo wa kimataifa wa Ureno, Allan mwenye umri wa miaka 29. ***(Express)***

**SILVA AWANIWA EVERTON**

CARLO Ancelotti anajaribu kumsajili mlinzi wa Paris St-Germain na Brazil, Thiago Silva kwa usajili huru, mara tu mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 utakapomalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Express)***

**BALE, ZIDANE BADO HAKIELEWEKI**

UHUSIANO wa Gareth Bale na kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane umefikia hatua isiyo na suluhu, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales mwenye umri wa miaka 30 bado ana furahia kukaa kwa miamba hao wa mji mkuu wa Hispania. ***(Marca)***

**MAJALIWA YA SANCHO HAYAJULIKANI**

MAJALIWA ya Jadon Sancho pale Borussia Dortmund bado hayajulikani baada ya kocha mkuu, Lucien Favre kukubali kwamba winga huyo Muingereza mwenye umri wa miaka 20 ni miongoni mwa wachezaji wanaoweza kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Sky Sports)***

**MUSTAFI AWANIWA BUNDESLIGA**

MLINZI wa kati wa Arsenal raia wa Ujerumani, Shkodran Mustafi mwenye umri wa miaka 28, amekubali kwamba anawaniwa na timu kutoka Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, huku majaliwa yake yakiwa hayajulikani kwa washika bunduki hao. ***(Star)***

**LEIPZIG YAKOMAA NA WERNER**

KOCHA wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann amesisitiza Timo Werner mwenye umri wa miaka 24, bado yupo kwenye mipango yake katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, licha ya fowadi huyo wa Ujerumani kufikia makubaliana na Chelsea. ***(Mirror)***

**CHELSEA YAONGEZA NGUVU KWA HAVERTZ**

CHELSEA imeongeza nguvu ya kumshawishi Kai Havertz, huku klabu yake ya Bayer Leverkusen ikisema haitazuia uhamisho wa kiungo huyo mwenye umri wa miaka 21, raia wa Ujerumani. ***(Kolner Stadt-Anzeiger)***

**ARTETA ATAKA LUIZ ASIONDOKE**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema David Luiz "ni mchezaji muhimu" na ana matumaini mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 33 ataongeza mkataba wake. ***(Reuters)***

# AZAM FC YASAKA MRITHI WA NGOMA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umeanika usajili wao na kusema wamepokea mapendekezo ya kusajili wachezaji watatu kwa ajili ya kuboresha kikosi chao kwa msimu ujao wa Ligi Kuu, ikiwamo kuziba pengo la mshambuliaji Donald Ngoma.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema wamepokea mapendekezo ya kocha Aristica Cioaba kusajili nyota watatu ambao wawili wa kigeni na mmoja mzawa.

Alisema katika nyota hao, watasajili mshambuliaji atakayechukuwa nafasi ya Ngoma aliyemaliza mkataba wa kukitumikia kikosi hicho.

"Mapendekezo tumepokea, usajili wetu utaangalia sehemu maalum ukizingatia nafasi ya ushambuliaji ndio maalum, na tutahakikisha tunapata watu ambao watafikia malengo yetu," alisema Popat.

Alisema wanasajili idadi hiyo sababu ya kocha wao huyo kuridhishwa na viwango vya baadhi ya nyota waliokuwapo na kutaka kuongezewa mikataba.

Popat alisema watakuwa makini katika usajili wao hasa safu ya ushambuliaji ambayo imekuwa na tatizo kwao.

"Msimu huu haturudii makosa, tunaboresha safu ya ushambuliaji na kuleta mtu atakayeimarisha nafasi hiyo kwa kupata idadi kubwa ya mabao kama misimu iliyopita," alisema Popat.



Kikundi cha ngoma za asili cha Michungwani wilayani Handeni kikitumbuiza juzi, wakati wa uzinduzi wa kituo cha kuweka mafuta kinachoendeshwa na kampuni tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (Tan Oil). **PICHA: OSCAR KASIMIRI**

# Waamuzi wajipanga kwa Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAMATI ya Waamuzi ya Shirikisho la Soka Zanzibar, ZFF, imesema wamuuzi wote wapo tayari kukabiliana na mechi za kumaliza msimu huu wa Ligi Kuu visiwani hapa ambayo ilisimama takribani miezi mitatu kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Akizungumza na Nipashe, Katibu Mkuu wa Kamati ya Waamuzi ambaye ni Kamishna wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Muhusini Ali Kamara, alisema waamuzi wote wameshajipanga kuendelea na msimu huu wa ligi kwa kufanya majukumu yao kama ilivyokuwa hapo awali.

Alisema waamuzi wote wamerudi katika mazoezi ya pamoja tangu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipotangaza tarehe ya kuendelea shughuli za michezo ikiwamo Ligi Kuu ya Zanzibar.

"Waamuzi wote hivi sasa wanaendelea kufanya mazoezi kama ilivyokuwa hapo awali na wapo tayari kuendelea na majukumu yao ya kurudi uwanjani kukabiliana na Ligi Kuu ya Zanzibar, ambayo ipo katika hatua ya mwisho," alisema.

Hata hivyo alisema kuwa waamuzi hao wataendelea kufuata sheria 17 za soka za msimu wa mwaka 2019/2020 kwa kumalizia msimu huu ikiwamo na marekebisho madogo ambayo Shirikisho la Soka la Kimataifa, FIFA, limeyafanya katika kipindi hiki cha ugonjwa wa corona.

## Namungo wazee wa sare tano mfululizo

**Na Adam Fungamwango**

SARE ya mabao 2-2 iliyopata timu ya Namungo dhidi ya Coastal Union Jumamosi kwenye Uwanja wa Mkwakwani mjini Tanga, imekuwa ni ya tano mfululizo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Namungo, yenye maskani yake mkoani Lindi ilicheza mechi yake ya kwanza baada ya mapumziko ya kupisha janga la ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona, bado haikuwa na dawa ya kutibu ugonjwa wa sare nne mfululizo ilizozipata kabla.

Mara ya mwisho Namungo kushinda mechi ilikuwa Februari 29 mwaka huu, ikiwa ugenini Uwanja wa Samora mjini Iringa, ikishinda mabao 2-1 dhidi ya wenyeji Lipuli, lakini baada ya hapo haijapata ushindi wowote wala kufungwa, zaidi ya sare. Timu hiyo inayokamata nafasi ya nne kwa pointi 51, baada ya kushinda ugenini, ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar ikiwa ugenini mjini Morogoro Machi 4, na ikaenda tena ugenini kucheza dhidi ya Polisi Tanzania na kutoka sare ya bila kufungana Machi 7 kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

Machi 10, ilikuwa ugenini kwa mara nyingine tena kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma mkoani Mara dhidi ya Biashara ikatoka sare ya bao 1-1, kabla ya kwenda nyumbani Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi na kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga, mechi iliyochezwa Machi 15.

## Ubalozi India waanzisha mashindano ya mazoezi

**Na Romana Mallya**

UBALOZI wa India nchini Tanzania katika kusherehekea Siku ya Kimataifa ya Yoga duniani, umeandaa mashindano ya mazoezi na kuhamasisha Watanzania kushiriki kwa kutuma video fupi zitakazowawezesha kushinda fedha taslimu.

Shindano hilo limeandaliwa na ubalozi huo kwa kushirikiana na Kituo cha Utamaduni cha Swami Vivekananda (SVCC).

Akizungumzia kuhusu shindano hilo jana jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa kituo hicho, Santhoth Raja, alisema washindi watakaopatikana watapata fursa ya kushindanishwa kidunia.

Alisema shindano hilo litaendeshwa kupitia mitandao ya kijamii ikiwamo ukurasa wao wa Facebook, Twitter na Instagram.

Alizitaja kurasa hizo kuwa ni pamoja na facebook.com/IndiaIntanzania/facebook.com/swami-Vivekananda-cultural-centre-Dar-es-Salaam.

Raja akielezea kuhusu shindano hilo mbele ya Balozi wa India nchini Tanzania, Sanjiv Kohli, alisema washiriki ni wa rika na jinsia zote ambao watatakiwa kutuma video fupi ya dakika tatu zitazoonyesha namna wanavyofanya mazoezi nyumbani.

Michezo
Alhamisi Juni 18, 2020
Nipashe



## Lewandowski: Sasa nataka taji la Uefa

HABARI UK 22



Kiungo wa Yanga, Haruna Niyonzima akiwatoka wachezaji wa JKT wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baina ya timu hizo jana, kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# YANGA YAPUNGUZWA KASI

## Vurugu zatawala, wawili walimwa kadi nyekundu...

**Na Somoe Ng'itu, DODOMA**

YANGA imerejea katika mwenendo wake wa kusuasua baada ya kukubali kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya JKT Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini hapa.

Kwa matokeo hayo, Yanga imefikisha pointi 55 wakati JKT Tanzania ikifikisha pointi 43 na kuendelea kujiondoa kwenye janga la kushuka daraja.

Michael Aidan ndiye aliyeifungia JKT Tanzania bao katika mchezo huo baada ya kumtizama kipa wa Yanga, Metacha Mnacha alivyokaa na kupiga upande wake wa kulia na hatimaye mpira kujaa wavuni moja kwa moja.

Bao hilo liliifanya JKT Tanzania iende mapumziko katika mchezo huo uliohudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe ikiwa mbele kwa goli 1-0.

Dakika ya 71, Patrick Sibomana aliwanyanyua mashabiki wa Yanga kwa kumalizia mpira uliotemwa na kipa wa JKT Tanzania, Mohammed Abdulrahman na kuisawazishia timu yake ambayo haikuonekana kukata tamaa licha ya kuwa nyuma kwa bao moja.

Hata hivyo mechi hiyo ilianza kwa kasi na timu zote zilikuwa zikishambuliana kwa kasi, lakini mabeki wa kila upande walionekana kufanya vema kazi zao kwa kuokoa mashambulizi yaliyokuwa yanatengenezwa zaidi kupitia pembeni, ilishuhudiwa nyota wawili, Lamine Moro wa Yanga na Mwinyi Kazimoto wa JKT Tanzania wakionyeshwa kadi nyekundu.

Mwamuzi Rudovick Charles kutoka Mwanza alilazimika kuwatoa nje nyota hao kutokana na kuianzisha vurugu ambazo zilisababisha mechi hiyo kusimamia kwa dakika nne.

Dakika ya tisa Ditram Nchimbi aliyeunganisha krosi kutoka kwa Mapinduzi Balama alikaribia kuifungia Yanga bao, lakini mabeki wa JKT Tanzania wakiongozwa na Edson Katanga walifanikiwa kuondoa hatari hiyo langoni mwao huku dakika tatu baada ya Katanga aliwahi tena kuosha shambulio lililofanywa na Haruna Niyonzima.

Kipa wa JKT Tanzania Mohammed alifanikiwa kupangua mpira wa adhabu uliopigwa na Niyonzima na kuinyima tena Yanga nafasi ya kufunga dakika ya 15, wakati Aidan akikaribia tena kufunga lakini krosi iliyopita dakika ya 23 ilitoka pembeni mwa goli la Yanga.

Dakika ya 32 Yanga ilipoteza nafasi nyingine ya kufunga baada ya Katanga na kipa Mohammed kufanikiwa kuokoa hatari langoni, huku Deus Kaseke akiwa jirani kumalizia krosi iliyopigwa na Juma Abdul wakati Mwinyi Kazimoto alipoteza nafasi ya kuifungia JKT baada ya shuti alilopiga kutoka nje akipokea mpira kutoka kwa Hassan Mwatelema dakika ya 41.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi na Yanga ilionekana kujipanga zaidi kwa kufanya mashambulizi mfululizo katika lango la wapinzani wao ambapo dakika ya 54 ilikaribia kupata bao kupitia Patrick Sibomana, lakini shuti lake lilikatika na kutoka nje ya kujaribu kazi nzuri iliyofanywa na beki, Adeyum Saleh.

Dakika ya 56 JKT Tanzania ilijibu mapigo kupitia kwa Adam Adam, lakini jitihada zake za kuwapangua mabeki wa Yanga zilisha baada ya mshambuliaji mwenzake wa Maafande hao, Mwatelema akiwa ameotea na kuwapa wapinzani wao ahueni huku Aidan akiijaribu tena kupiga lakini Metacha alifanikiwa kupangua shuti hilo la dakika ya 58.

Adam aliendelea kuisumbua Yanga lakini shuti lake la dakika ya 67 akimalizia pasi fupi ya Kazimoto liliishia mikononi mwa Metacha, huku dakika mbili baadaye Sibomana tena ameshindwa kuliona bao la JKT Tanzania na kwenda kufanya mashambulizi nje ya lango.

JKT Tanzania; Abdulrahman Mohammed, Michael Aidan, Abdallah Waziri/ Danny Lyanga (dk 89), Frank nchimbi, Edson Katanga, Jabir Aziz, Kelvin Nashon/ Mohammed Rashid (dk 63), Mwinyi Kazimoto, Shabani Mgandila/ Hafidh Mussa ( dk 72), Hassan Mwatelema na Adam Adam/ Edward Songo (do 83).

Yanga; Metacha Mnata, Juma Abdul, Adeyum Saleh, Lamine Moro, Said Juma, Kelvin Yondani, Feisal Salum, Haruna Niyonzima/ David Molinga (dk 80), Ditram Nchimbi/ Mrisho Ngassa (dk 88), Mapinduzi Balama/ Patrick Sibomana ( dk 53) na Deus Kaseke/ Yikpe Gislain (dk 67).

## Viongozi wajichanganya michango Ndanda

**Na Faustine Feliciane**

SIKU chache baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, kutoa kauli ya kutaka kuchangisha wadau wa mkoa huo kuisaidia klabu ya Ndanda FC, uongozi wa klabu hiyo umeibuka na kudai mambo yanaenda vizuri na hakuna shida kubwa.

Ilielezwa Ndanda inahitaji kiasi cha Sh. milioni 72 kwa ajili ya kuisaidia kumaliza ligi vizuri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msemaji wa klabu hiyo, Idrisa Bandali, alisema kuwa hakuna suala la kupitisha 'bakuli' klabuni hapo na kila kitu kinaenda sawa.

Aidha, alimshangaa kocha wa timu hiyo Meja mstaafu Abdul Mingange juu ya kauli yake kuwa mshahara ni tatizo kwa wachezaji wake.

"Suala la michango hakuna, uongozi haujaamua hilo na halipo mezani kwangu, ninachofahamu timu inaendelea vizuri na kila kitu kipo sawa hakuna tatizo lolote," alisema Bandali na kuongeza, "hiyo taarifa sio ya kweli, timu ipo kambini kujiandaa na mchezo wetu ujao dhidi ya Biashara, hakuna malalamiko yoyote kutoka kwa wachezaji kila kitu kipo sawa," alisema.

## Sven awapa mzuka wa ubingwa Simba

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema mipango yao ni kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Bara na Kombe la FA, hivyo huwaangalia wanacheza na timu iliyopo nafasi ipi kwenye msimamo wa ligi.

Kocha huyo aliyazungumza jana jijini katika mazoezi yaliyofanyika Mo Simba Arena na kwamba wachezaji wapo tayari kwa ajili ya mechi zote zilizobaki ikiwa ni pamoja na Mwadui FC, utakaopigwa Jumamosi hii Uwanja wa Taifa.

Alisema anafikiri kuna kazi kubwa kwenye mechi zao zilizobakia, hawatatazama wanacheza na timu iliyopo nafasi ipi, anachokifanya ni kutafuta ushindi.

"Kwa namna ninavyoiona sasa ligi imekuwa na ushindani mkubwa uwanjani, tunapambana kupata matokeo bila ya kujali tunakutana na timu iliyopo nafasi ipi," alisema Sven.

Alisema matokeo ya mechi iliyopita ni maandalizi ya mechi ijayo hivyo amefanyia kazi upungufu wa kikosi chao kwa ajili ya kutafuta ushindi katika mchezo dhidi ya Mwadui.

"Tumefanyia kazi upungufu wa mechi iliyopita ambayo tumepoteza pointi mbili pamoja na kuboresha zaidi sehemu iliyopo imara ili kutafuta ushindi na kufikia malengo yetu kutwaa ubingwa wa ligi," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >